# NINI KILITOKEA UYAHUDI MWAKA 70 B.K.?

**[WHAT HAPPENED IN A.D. 70?]**

Na Edward E. Stevens

*Dibaji na David Chilton*

*Tafsiri ya Kiswahili na*
*Respicius Kilambo Luciani*

*… Siku zitakujilia, adui zako watakapojenga boma litakalokuzunguka, utazingirwa pande zote; watakutupa chini, wewe pamoja na watoto wako ndani ya kuta zako; wasikuachie jiwe juu ya jiwe; kwa kuwa hukuyajua majira ya kujiliwa kwako. Luka 19:43-44*

## MAELEZO MAFUPI YA MCHAPISHAJI

Chapisho hili, *Nini Kilitokea [Uyahudi] Mwaka 70 B.K.*, la Edward Stevens limechapishwa upya na Nierton Particular Baptists kwa lengo la kuuendeleza na kuupa kipaumbele ukweli.

Migongano kati ya Ukelvini na Uarmini ni ya lazima kwa ajili ya kuonyesha mtazamo sahihi wa Soteriolojia (mafundisho ya wokovu). Mara baada ya kuthibitisha utaratibu na njia ya wokovu kwa kutatua mgogoro kati ya mitazamo hiyo miwili, suala muhimu la Eskatolojia (mafundisho ya mambo ya mwisho / hatma) yanapaswa kupatiwa ufumbuzi. ***Hii ni njia ya kila Mkristo***.

Kitabu hiki kinampa msomaji utangulizi wa mtazamo wa kutimizwa kwa unabii ambapo kitabu cha Ufunuo kinachukuliwa kuwa ni fasiri juu ya mafundisho ya Bwana Yesu katika mlima wa mizeituni na si kama wale wenye mtazamo wa wakati wa siku za mwisho, kuinuka kwa mpinga-kristo, urejesho wa taifa la [kimwili la] Israeli na urejesho wa mfumo wa kutoa dhabihu wa Walawi wa Uyahudi.

Tumeweka [humu] orodha ya vitabu vya mafundisho ya ziada kwa wale wenye shauku ya kuielewa dini ya Kikristo.

Kila kitabu kinaweza kupatikana kwa njia ya kubonyeza [hyper]link ya maandishi ya buluu ambayo itakupeleka mahala iliko nakala katika mfumo wa PDF wa kitabu hicho. Orodha hii ina vile vitabu ambavyo tumevikusanya katika takriban miaka 50 iliyopita ambavyo ni [vitabu] vya Kikristo vilivyoandikwa na Wakristo kabla ya karne ya 19, na nukuu na marejeo yake ya Biblia yametoka katika tafsiri Iliyoidhinishwa ya Mfalme Yakobo [ya 1611]. Tafadhali soma chapisho letu, What Version, Authorised or Revised by Philip Mauro, iliyo katika orodha mwishoni mwa kitabu hiki. Chapisho hili linamwezesha mtu asiyejua suala muhimu la tafsiri za Biblia kufanya uamuzi wake mwenyewe kuhusu tafsiri ipi ya Kiingereza cha kisasa ni ya kuaminika, kati ya tafsiri nyingi zilizoko.

Biblia ya Kiingereza, Tafsiri Iliyoidhinishwa, imekuwa ikitumiwa na Wakristo kwa miaka takriban 400 sasa tangu kipindi cha Reformation, na imetafsiriwa kutoka katika hati (manuscripts) nyingi za kuaminika za Kiyunani. Tafsiri zote za kisasa zimetokana na hati zisizoaminika, hivyo nakushauri utumie ile ***1611 King James Version***.

## TABARUKU NA EDWARD STEVENS

Kitabu hiki kimeandikwa kwa heshima ya wakufunzi waaminifu na wacha Mungu wa Sunset International Bible Institute (seminary) walionifundisha jinsi ya kufasiri Maandiko, na kunipa misingi ya mfumo wa imani katika ujumla wake kama inavyofunuliwa katika Biblia. Ninaomba [kwa Mungu] kwamba juhudi zao katika kuwafundisha watu waaminifu zipate thawabu ya kuzaa matunda mengi mema [jinsi] wanavyoingia mbinguni katika vizazi vyote kutoka enzi hata enzi (Waefe. 3:21). Wamekuwa ni mfano wa kuigwa, na wamedhihirisha utukufu wa Mungu. Ninaomba Mungu awazidishie neema Zake za kiroho katika “kipimo sahihi, kilichoshindiliwa, na kutikiswa, hata kikafurika”.

**DIBAJI na DAVID CHILTON**

Katika kijitabu hiki, Edward E. Stevens anadhihirisha kwa wazi na bila shaka yoyote kwamba Bwana wetu Yesu Kristo alitabiri Kurejea Kwake katika kizazi cha wale waliokuwa wakimsikiliza katika karne ile ya kwanza. Ukweli huu unawaweka Wakristo katika mgongano wa kuchagua: kama Kristo alikosea katika utabiri wake (kama ambavyo waliberali wamekuwa wakidai kwa miongo kadhaa sasa), basi tuna tatizo kubwa kuliko mdahalo tu wa kiteolojia kuhusu mambo ya mwisho – eskatolojia – maana yake ni kwamba hatuwezi kumtumainia Bwana Yesu kwa ajili ya wokovu wetu pia! Kama hatuwezi kumwamini Bwana Yesu katika Matthew 24, hatuwezi kumwamini katika Yohana 3:16 pia! Kama ambavyo Dr. R. C. Sproul, Sr. alivyowahi kusema, “Kama Yesu ni nabii wa uwongo, [basi] imani yangu ni batili.”

Lakini Bw. Stevens anadhihirisha kwamba Yesu alitimiza ahadi Yake, kwa uhakika kabisa, katika “dhiki kuu” ya mwaka 70 B.K. ambapo Mungu alifungua ghadhabu Yake ya ki-agano dhidi ya Israeli, kitendo ambacho alikuwa akitishia kukifanya kwa karne kadhaa katika Agano la Kale, na akatimiza mahususi dhidi ya Israeli ya karne ya kwanza katika Agano Jipya.

Mimi nimevutiwa mahususi na hoja zake mbili: Kwanza, ni chati / jedwali lake linaloonyesha upatanifu wa hotuba mbili za Kristo katika Matthayo 24 na Luka 17, na kwamba mgawanyo wowote wa Matthayo 24 katika “Ujio wa Pili” na “Ujio wa Tatu” si halali, ni hafifu, na unaleta mkanganyiko tu. Maandiko yanatabiri na kutufundisha kuhusu Ujio wa Pili (Waebr. 9:28) – na hakuna Ujio wa Tatu!

Pili, Stevens analichukua azimio la Kristo katika Luka 21:22 na kulipeleka mpaka mwisho wake: “Yesu alisema kwamba unabii wote katika Agano la Kale utatimia na kumalizika pale Yerusalemu utakapoangamizwa.” Nilipozidi kutafakari ukubwa wa maana na matokeo ya maneno hayo ya Yesu, ndivyo nikazidi kuelewa umuhimu wake wa kimapinduzi katika eskatolojia. Bila kukosa, kila tukio lililotabiriwa na manabii wa Biblia lilitimia katika kizazi kile, kama Bwana Yesu alivyoahidi (Matt. 16:27-28; 24:34).

Stevens anaboresha tasnifu yake ya Kibiblia kwa kunukuu mashuhuda kutoka karne ya kwanza kama Josephus, mwana-historia wa Kirumi Tacitus, vitabu vya Talmud, na vitabu vya mwana-historia wa Kikristo Eusebius, huku akitoa hoja ya nguvu kwamba Ujio wa Pili ulitokea mwaka 70 B.K.

**David H. Chilton, M. Div., Ph. D.**
September 23, 1996
Diamond Springs, California

Vitabu vingine vya Chilton juu ya eskatolojia ya ki-preterist ni: *Paradise Restored* (1985); *Days of Vengeance* (1987); *The Great Tribulation* (1987)

## DIBAJI

Kitabu hiki kinatoa mtazamo wa unabii wa Biblia ambao watu wengi wamefaidika nao sana katika masomo yao ya Biblia. Kinafasili vitendawili vya siku za mwisho ambavyo kwa muda mrefu vimewasumbua wanazuoni wa unabii wa Biblia. Ni mtazamo thabiti (usio na mgogoro) ambao unakifanya kitabu cha Ufunuo kuwa rahisi zaidi kuelewa. Kinathibitisha wakati ambao uandishi wa vitabu vya Agano Jipya ulikamilika, kinaangamiza shambulizi la waliberali kuhusu ukweli kwamba chanzo cha [vitabu vya Agano Jipya] ni Mungu Mwenyewe, na kinaendana na mafundisho mengine sahihi kuliko yale ya kimapokeo. Na hakuna mlegezo katika kanuni muhimu za Biblia zinazohimili imani ya Kikristo.

Ufunguo wa kuelewa aya yoyote ya Maandiko siku zote ni kufahamu muktadha wa kihistoria ambamo aya hiyo iliandikwa (walengwa wa aya hiyo). Miaka 2000 ijayo kutoka sasa, historia yetu, utamaduni, siasa na lugha vitakuwa vimebadilika sana. Fikiria tu ulazima wa mtu kujifunza lugha ya kale inayoitwa “American English” ili aweze kusoma magazeti ya USA ya leo. Kama mtu huyu akiona moja kati ya vikaragosi vya kisiasa vinavyochorwa leo vyenye michoro ya punda na tembo, atawaza nini? Ni kwa njia ipi ataelewa maana yake? Si tu kwamba mtu huyu atalazimika kujifunza lugha, bali pia utamaduni, historia, siasa, na uchumi wetu. Mbinu hizo hizo zinatumika katika kujifunza Biblia. Kama tunataka kuelewa “punda na tembo” (wanyama, kahaba, joka, nk) wanaashiria nini katika Kitabu cha Ufunuo, basi tunapaswa kujifunza kwa uangalifu na kwa makini lugha, historia, uchumi na siasa za Karne ya Kwanza. Kwa hakika, kanuni za kweli zilizo muhimu kwa ajili ya wokovu zimeandikwa katika lugha rahisi na ya moja kwa moja ambayo kila mtu anaweza kuelewa. Lakini kuna maandiko mengi ndani ya Biblia ambayo ni “magumu kuelewa” (cf 2Pet. 3:16), na unabii [wa Biblia] ni moja kati ya mambo ambayo yanapaswa kusomwa kwa kuzingatia sana muktadha wake wa kihistoria na kiutamaduni (walengwa wa mwanzo wa maandiko hayo).

Moja kati ya malengo makuu ya kijitabu hiki ni kutoa uchunguzi wa karibu zaidi wa mazingira ya kihistoria yaliyokuwako wakati wa uandishi wa Agano Jipya. Wengi wameona kwamba inasaidia kuweka kando (angalau kwa muda tu) utitiri wa maoni ya kukisia [tu] juu ya kitabu cha Ufunuo, na kutazama mbadala wa kihistoria zaidi, ambao ni kwamba kitabu cha Ufunuo kililengwa kwa kanisa la karne ya kwanza, na kilikuwa na umuhimu wa juu kabisa kwao. Kilitoa tahadhari kuhusu matukio yaliyokuwa karibu kabisa kutokea katika kizazi chao, na kiliwaandaa kwa ajili ya tukio kubwa lenye kuleta simanzi la “Dhiki Kuu” (Tribulation) na matukio mengine yaliyohusiana na Mwisho wa Enzi ya Kiyahudi.

Wakana-Mungu (atheists), wenye kushuku kwamba [labda] Mungu hayupo (skeptics / sceptics), Wayahudi, Waislamu, na wakosoaji wa kiliberali wa Biblia, wote wanaitumia ***dhana*** kwamba ati matukio yale ya siku za mwisho hayakutokea katika Karne ya Kwanza katika kampeni yao ya kuhujumu uadilifu na ukamilifu wa Kristo na vitabu vyote vya Agano Jipya. Wengi kati ya watu hao hutoa kauli za kejeli wakisema, “***Yesu anarudi lini?!***” au “***Jambo hili halitotokea mpaka Yesu arudi!***” Wakimaanisha ***kamwe!***

Wayahudi ambao si Wakristo wanacheka na kukebehi katika dhana yao kwamba ubashiri wa Bwana Yesu haukutokea, na wanaitumia dhana hii kudai kwamba Yesu si Masihi. Baba zao katika mwili walimkataa Yesu katika Ujio wake wa Kwanza kwa sababu hakutimiza unabii wa Agano la Kale katika namna ya kimwili na kitaifa / kizalendo waliyokuwa wakiitarajia, ingawa Yesu aliwaambia bayana kwamba ufalme Wake haukuwa wa ulimwengu huu, na kwamba badala yake [ufalme Wake] umo ndani yao. Lakini inaelekea kwamba, leo hii, wengi wanaoutarajia ufalme [wa kimwili] wa Kristo katika siku za usoni wanategemea aina hiyo hiyo ya ufalme wa kimwili na kitaifa kutokea

katika siku za usoni, katika “Ujio Wake wa Pili”. Je, wanafanya kosa lile lile kuhusu ujio Wake wa Pili ambalo Wayahusi walilifanya kuhusu Ujio Wake wa Kwanza? Bwana Yesu alisema mara nyingi kwamba ufalme Wake “si wa dunia hii” na kwamba “hautokuja kwa kuona kwa macho”. Ni ufalme wa kiroho na upo kati yetu, umekwishafika. Tunaishi ndani ya ufalme huu. Wayahudi wasio Wakristo na Wakristo wanaoutarajia katika siku za usoni wanapaswa kuliona hili.

Hatimaye Wakristo wameanza kutafuta mbadala wa tafsiri yenye makosa ya matarajio ya siku za usoni ya ufalme huu. Kijitabu hiki kinawakilisha mtazamo unaoitwa “PRETERIST”. Maana rahisi ya neno “preterist” ni “imekwishatimia hapo zamani”. Inamaanisha kwamba Kristo amekwishatimiza ahadi Yake ya kurudi na kukamilisha ukombozi katika Yeye na katika ufalme Wake wa kiroho unaoendelea (kanisa). Tunapaswa kuwa kama wale Waberea waadilifu na “kutafiti maandiko kila siku ili kuona kama mambo hayo ni kweli.” Unaweza ukaihitaji Biblia yako pembeni yako wakati unasoma kitabu hiki.

Edward E. Stevens<br>Bradford, Pennsylvania<br>April 17, 2018

Note Well: Ndugu msomaji, utakuja kuona mwenyewe kwamba Ukristo, katika maana yake ya Agano Jipya, bado ni dini changa, kwa maana ya kwamba sehemu kubwa sana ya Agano Jipya ***bado*** haijaeleweka kwa usahihi na Wakristo wenyewe wengi. Hii haina maana kwamba BWANA hapati mavuno Yake, kwani yeye mwenyewe alisema kwamba katika kila enzi, Yeye amejiwekea mabaki Yake!


NB: Dear reader, you will come to realize that Christianity, in its New Teastament sense, is still a young religion, because a large part of the New Testament itself is ***yet*** to be understood by a large part of Christians themselves. However, this does not mean that the LORD does not get His harvest, for He himself said that He has reserved for Himself a harvest (a remnant) in every generation!

R. Kilambo.

**Yaliyomo**


MAELEZO MAFUPI YA MCHAPISHAJI 2
TABARUKU NA EDWARD STEVENS 2
DIBAJI NA DAVID CHILTON 3
DIBAJI 4
MZINGO WA JESHI LA RUMI DHIDI YA YERUSALEMU MWAKA 70 B.K. 7
1 NINI HASWA KILITOKEA MWAKA 70 B.K.? 8
2 JE, YESU NA WAANDISHI WA AGANO JIPYA WALIKOSEA? 9
3 KAULI ZA “YUKO KARIBU!” ZILIONGEZEKA MWISHONI 11
4 JOSEPHUS NA HISTORIA YA KARNE YA KWANZA 13
5 AINA 5 ZA KUTIMIA ZILIZOTAJWA KATIKA VITABU VYA JOSEPHUS 14
6 JOSEPHUS ANATAJA ‘SIKU NA SAA’ 15
7 UJIO “MDOGO TU” MWAKA 70 B.K.? 16
8 TAREHE YA UANDISHI WA KITABU CHA UFUNUO 17
9 TAREHE YA KITABU CHA UFUNUO KABLA YA 70 B,K, 20
10 NABII DANIELI NA UFUNUO 21
11 MATTHAYO 24 NA UJIO WA PILI 22
12 KUHUSIANA NA JEDWALI 22
13 KUTOGAWANYIKA KWA HOTUBA YA MLIMA WA MIZEITUNI 24
14 VITABU VYOTE VYA AGANO JIPYA VILIANDIKWA KABLA YA 70 B.K. 27
15 JE, BADO TUMO KATIKA SIKU ZA MWISHO? 29
16 JE, UFALME WA MILELE ULIKUJA? 29
17 JINSI GANI TUTAFSIRI LUGHA YA UNABII? 31
18 JE, AGANO LA KALE LILIBASHIRI UJIO WA PILI? 33
19 KWA NINI WAYAHUDI WALIANGAMIZWA? 35
20 VIPI KUHUSU ISRAELI YA LEO? 36
21 HII INABADILISHA VIPI MTAZAMO WETU WA ULIMWENGU? 37
22 VIPI KUHUSU SISI WAKATI HUU? 37
23 MAISHA YALIVYO SASA KATIKA UFALME WA MILELE 39
24 TUMAINI BORA ZAIDI LA UZIMA WA MILELE 39
25 HITIMISHO 40

MZINGO WA JESHI LA ROMA DHIDI YA YERUSALEMU KATIKA MWAKA 70 B.K.



## 1 NINI HASWA KILITOKEA MWAKA 70 B.K.?

Sote tunahitaji kujikumbusha (au kuelimishwa) kuhusu historia ya Karne ya Kwanza. Matukio fulani muhimu sana yalitokea wakati ule, na ni nadra sana kusikia habari zake, pia ni nadra zaidi kuelezwa juu ya umuhimu wake. Katika mwaka 66 B.K. Wayahudi walifanya uasi dhidi ya utawala wa Rumi. Mambo mengi yalichangia katika kusababisha uasi huu, kwa upande wa Rumi, na kwa upande wa Uyahudi. Jeshi la Rumi likaja kuuzima uasi huu, na hadi kufikia kiangazi cha mwaka 70 B.K. walikuwa wamefanikiwa kuukamata mji wa Yerusalemu na kuuzima uasi. Mji wa Yerusalemu ukafanywa nyara na kuporwa mali zake na ukachomwa moto, na hekalu likabomolewa na kuchomwa moto.

Yesu Kristo alibashiri matukio haya yote takriban miaka 40 kabla. Utabiri Wake wote ulikuja kutokea, kama alivyobashiri. Taifa la Kiyahudi na mfumo wake wa kutoa dhabihu vilibomolewa kabisa kiasi kwamba Wayahudi hawajaweza tena kulijenga hekalu na kuanzisha upya mfumo wa kutoa dhabihu katika namna yoyote thabiti tangu wakati ule. Ma-rabbi wengi wanautaja mwaka 70 B.K. kama “Mwisho wa dini ya Kibiblia ya Uyahudi”. Tukio hili lilikuwa na umuhimu mkubwa zaidi kwa Wakristo, kama tutakavyoona.

[Wakati ule] Wakristo walikuwa wakitazamwa kama dhehebu lingine tu [mojawapo] la dini ya Uyahudi (Judaism). Na madhehebu mengine (Wafarisayo, Wasadukayo, Waesene, nk) walikuwa wakiwatesa sana Wakristo katika juhudi za kuwaangamiza kabisa kabla hawajasimama na kuthibitika. Lakini mwaka 70 B.K. ulibadilisha hayo yote. Baada ya mwaka 70 B.K., Wakristo hawakuchukuliwa tena kama dhehebu mojawapo la dini ya Wayahudi. Madhehebu mengine yote yalishiriki katika uasi [ule] dhidi ya Rumi, isipokuwa Wakristo wa Kiyahudi. Kwa kuwa walikumbuka ubashiri wa Yesu kuhusu mambo haya na tahadhari Yake [kwao] ya kutojihusisha na mambo hayo, Wakristo wa Kiyahudi waliondoka Yuda (Matt. 24:15-21; Marko 13:14-16,19-20). Kwa kuwa hawakushiriki katika uasi ule, Wakristo wa Kiyahudi walijitofautisha na Wayahudi wengine. Wakristo walikuwa wakiendelea katika ufalme wa kiroho, si wa kimwili, dondoo ambayo tunapaswa kuikumbuka siku hizi, licha ya maombi mengi ya Ma-zayonisti ya kututaka [Wakristo] tuwasaidie.

Kwa kuwa haikuwezekana kutimiza Sheria baada ya uharibifu wa hekalu, mabishano kuhusu tohara na kutimiza matakwa ya Sheria yakapungua. Taifa la Kiyahudi liliharibiwa kwa kiwango kikubwa sana kiasi cha kwamba halitokuwa na nguvu za kutosha kuwa tishio kwa wafuasi wa Kristo.

Kuangamia kwa Yerusalemu kwa hakika kulionyesha kwamba Ufalme ulikuwa umechukuliwa kutoka Uyahudi na kukabidhiwa kwa wafuasi wa Kristo (tazama Matt. 21:23-43). Kulitoa ushuhuda wa mwisho kuhusu Yesu alikuwa nani. Kulionyesha dhahiri kwamba Mungu hakujali kuhusu ufalme wa kimwili kwa ajili ya Wayahudi, bali alikuwa Anajishughulisha na ufalme wa kiroho wa Yesu juu ya mataifa yote. Yesu aliwaambia watesi wake kwamba wataona kwa macho yao wenyewe kitu ambacho kitathibitisha madai Yake ya kuwa Masihi (Matt. 26:63,64). Uthibitisho huo ulikuja katika mwaka 70 B.K. pale taifa la Kiyahudi lilipoangamizwa. Wayahudi wa kizazi kile ni lazima walikuwa waovu kweli kweli kustahili Mungu aamue kuwaangamiza katika namna ile. Uharibifu ule uliwafungua macho mataifa mengine yaliyokuwa katika ulimwengu ule wa Rumi pia. Uliwathibitisha wafuasi wa Kristo kuwa ni Israeli [mpya] halisi ya Mungu.

Uharibifu wa Israeli ulikuwa mkubwa kuliko vile wengi wetu tunavyofikiri. Yesu alibashiri kwamba uharibifu utatokea katika kizazi kile, lakini pia uharibifu ungetokea katika “ujio” Wake na katika “mwisho wa enzi / dahari” (Matt. 24:3). Mambo haya yote yalipangwa kutokea katika “kizazi” kile cha karne ya kwanza (Matt. 24:34). Kuna aya nyingi sana zinazofundisha kwamba Yesu alikuwa

anarudi katika ile karne ya kwanza. Soma na ujifunze aya zifuatazo kwa uangalifu na utaona zinazungumzia majira ya kurejea kwa Bwana Yesu: Yak. 5:8ff; 1 Pet. 4:7; Matt. 10:23; 16:27ff; War. 13:11ff; Waebr. 10:37; 1 Yoh 2:18; Ufu. 1:1,3; 22:6,7,10,12,20. Aya hizi na nyingine nyingi zinaweka wazi kwamba Yesu angerudi katika kizazi kile. Kile tunachokiita katika mapokeo yetu "Ujio wa Pili" kilitokea wakati huo katika kizazi kile Yerusalemu ilipoangamia. Soma Waebr. 9:26-28 ambapo tunaona kwamba ilipangwa Bwana Yesu aje tena "si kwa ajili ya kubeba dhambi" bali kwa ajili ya kuwaokoa wale waliokuwa wakisubiri kwa shauku, na kuwahukumu wale waliomkataa na kuasi (Waebr. 10:25-37). Kauli hizi za majira zinazohusiana na ukaribu wa kurejea kwa Kristo haziwezi kuchukuliwa katika namna yoyote nyingine bila ya kutia shaka katika ukamilifu na uadilifu wa maandiko ya Agano Jipya. Ili uone aya zaidi zinazofundisha kwamba Ujio wa Pili wa Kristo ulipangwa kutokea katika karne ya kwanza, tazama orodha zilizoko katika kurasa zinazofuata.

Kitabu cha ufunuo kinasimulia madhila ya kutisha yaliyowasibu Wayahudi katika vita yao dhidi ya Warumi (66-70 B.K.). Mpambano wa Armageddon ulitokea katika mwaka 70 B.K. wakati Mungu alipotumia jeshi la Rumi kusitisha mateso ya Wakristo yaliyofanywa na Wayahaudi. Kitabu cha Ufunuo (pamoja na vitabu vingine vya Agano Jipya) viliandikwa kabla ya uharibifu wa Yerusalemu, na kipaji cha kunena na kuandika [unabii] kwa uweza / ufunuo wa Roho Mtakatifu kilikoma mwaka 70 B.K. Kila kitu kilichokuwa muhimu kwetu kufahamu kuhusu Ufalme kilikwishafunuliwa kufikia wakati huo, hivyo kanuni za Maandiko zilikamilika. Ufalme ulikuwa umethibitishwa chini ya uongozi wa Kristo, na adui za Kristo (wale waliomkataa na kuwatesa wafuasi Wake) walikwishaangamizwa. Unabii wote wa Agano la Kale uliohusu Ufalme na kurejea kwa Kristo ulikwishatimizwa (Luka 21:22,31).

## 2 JE, YESU NA WAANDISHI WA AGANO JIPYA WALIKOSEA?

Mtazamo wa ki-preteristi unakanusha kabisa hoja kuu zinazotumiwa na wa-liberali na watia-shaka dhidi ya uadilifu na ukamilifu wa Kristo na wa Agano Jipya. Kwa mfano, Albert Schweitzer, mwana-teolojia maarufu wa kiliberali, katika kitabu chake, The Quest for the Historical Jesus, ametumia maneno mengi sana akiandika ukweli kwamba Kristo alibashiri ujio Wake wa Pili katika wakati wa kizazi chake ("katika kizazi hiki" kabla ya "kifo cha baadhi ya waliosimama pale"). Schweitzer akahitimisha kwamba Yesu alishindwa kurejea katika wakati alioahidi.

Halafu Bertrand Russell, katika kitabu chake Why I am not a Christian, akaitumia dhana hii bandia ya kushindwa kurejea kwa Kristo katika kumfedhehesha Kristo na kuukana Ukristo. Wakosoaji wengi kama hawa (wakana-mungu, waliberali, watia-shaka, Wayahudi, Waislamu) wanaitumia orodha ile ile ya aya za Agano Jipya katika madai kwamba Yesu ni nabii wa uwongo, na kwamba waandishi wa Agano Jipya walikosea na hivyo hawakuongozwa na Roho Mtakatifu. Hapa chini kuna orodha ya aya za Maandiko ambazo watu hawa wanazitumia katika mashambulizi yao dhidi ya kuaminika kwa Kristo na Agano Jipya. Waandishi wote wanane wa Agano Jipya wanawakilishwa hapa. Ili uuone uzito wa ukosoaji wao, soma kila moja kati ya aya hizi katika Biblia yako na uzitafakari katika muktadha wa historia ya karne ya kwanza:

### A. Ujio wa Pili Ulikuwa <u>Karibu</u> katika Karne ya Kwanza:

- Matt. 10:23 (hawatamaliza kuizungukia miji kabla hajarudi)
- Matt. 16:27-28 (*na aya zinazofanana) (baadhi ya walio hai wataushuhudia Ujio)
- Matt. 24:33-34 (*na aya zinazofanana) (kabla kizazi hakijaisha)
- Matt. 26:64 (*na aya zinazofanana) (viongozi wa Kiyahudi kuuona Ujio)
- War. 13:11-12 (saa ya kuamka imekaribia; siku imefika)

- War. 16:20 (hivi punde mtamponda shetani chini ya miguu yenu)
- 1Wakor. 7:26-31 (muda ni mfupi; ulimwengu unapita)
- 1Wakor. 10:11 (mwisho wa enzi umefika)
- 2Wathess.2:7 (siri ya uasi)
- Waebr. 1:2 (siku za mwisho zimefika)
- Waebr. 9:26 (kukamilishwa kwa enzi – enzi *pl*)
- Waebr. 10:25 (siku inakaribia)
- Waebr. 10:37 (Anakuja "muda mfupi ujao")
- Yak. 5:7-9 (Ujio wa Bwana u karibu) cf. Wafi. 4:5
- 1Pet. 1:20 (nyakati za mwisho zimefika)
- 1Pet. 4:7 (mwisho wa mambo yote umefika)
- 1Pet. 4:17 (wakati wa hukumu kuanza) cf. Ufu 3:10
- 1Yoh 2:8,17,18 (ilikuwa saa ya mwisho)
- Yuda 18,19 (wenye kudhihaki wa wakati wa mwisho)
- Ufu. 1:1-3; 22:6, 10 (hayana budi kutokea punde; u karibu)
- Ufu. 22:7, 12, 20 (Kristo anakuja punde) cf. Ufu. 2:16; 3:11

**B. Mifano Kuhusu Mwisho wa Dahari & Ujio wa Pili:**

- Matt. 13:24-43 Mfano wa Mpanzi
- Matt. 13:47-50 Mfano wa Nyavu ya Kuvulia Samaki
- Matt. 21:33*ff (Mk. 12:1ff; Lk. 20:9ff) Shamba la mizabibu
- Matt. 22:1ff (Lk. 14:16ff) Mfano wa Karamu ya Harusi
- Luka 19:11-17 Mfano wa Watumishi Kumi
- Matt. 25 Mfano wa Wari Kumi na Talanta
- Luka 13:6-9 Mfano wa Mtini Usiozaa

*ff – maana yake na aya zinazofuata

**C. Kauli Nyingine Kuhusu Uharibifu na Ujio:**

- Matt. 3:7-12 (Lk. 3:7-17; Lk. 12:49)
- Matt. 10:17-34 (Lk. 10:3-21; Lk. 12:11-56)
- Matt. 23:29-24:44 (Mk. 13; Lk. 17:20-37; Lk. 21)
- Luka 11:42-52; 12:49; 13:33-35; 19:41-44; 23:27-31

Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "*Kuna baadhi wanasimama hapa ambao hawataonja mauti hata watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika ufalme Wake*" (Matt. 16:28). Paulo aliwaambia Warumi kuwa "*Saa ya wao kuamka ilishafika*", kwa sababu, "*Usiku unakaribia kwisha, siku mpya I karibu*" (War. 13:11,12). Paulo pia aliwakumbusha Wakorintho kwamba walikuwa wakiishi katika wakati ambao "*Ukamilisho wa enzi (pl) umefika*" (1 Wakor. 10:11). Paulo alisema kwamba huduma ya Kristo hapa duniani ilikuwa katika wakati ambao enzi zilikuwa zinakamilishwa (Waebr. 9:26). Yakobo aliandika (mwaka 62 B.K. muda mfupi tu kabla hajawa mhanga wa Kristo), "*Ujio wa Bwana umekaribia"* na "*Hakimu amesimama mlangoni*" (Yak. 5:8,9). Naye Petro, akiandika muda mfupi baadaye alisema, "*Mwisho wa mambo yote umekaribia*" na "*Ni wakati wa hukumu kuanza*" (1 Pet. 4:7,17). Yohana (aliyeandika kitabu cha Ufunuo) anasema katika waraka wake wa kwanza, "*Dunia inapita*" na "*Hii ni saa ya mwisho*" (1Yoh. 2:17,18). Katika kitabu cha Ufunuo anasema katika sehemu mbili tofauti kwamba mambo yote yanayofunuliwa katika kitabu hiki "*yatatokea katika muda mfupi ujao"* na kwamba wakati wa kutimizwa kwake ulikuwa "*umefika*" (Ufunuo 1:1,3; 22:6,10). Yesu alithibitisha tena na tena katika kitabu cha Ufunuo kwamba Ujio Wake ungetokea "*punde"* tu (Ufunuo 22:7,12,20).

Waandishi wa Agano Jipya walifundisha kwamba kurejea kwa Kristo *kungtokea katika wakati wa uhai wao!* Hakukua hata na chembe ya shaka katika mioyo yao. Hawasemi "labda!" au "inawezekana!" Wanathibitisha kwa uhakika kwamba Ujio na Mwisho umekaribia, na kwamba baadhi yao watakuwa wangali hai kuuona:

4:16 Kwani Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni na sauti kuu itapaazwa, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu: nao waliokufa katika Kristo, watafufuliwa kwanza;
4:17 Ndipo sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani: na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.
4:18 Basi, peaneni faraja kwa maneno haya.
1 Wathess. 4:16-18 (Tafsiri kutoka KJB)

Wakati kizazi kile cha kwanza cha Wakristo kilivyoanza kuelekea mwisho wake, vitabu vichache vya mwisho vya Agano Jipya vikakamilika. Si tu kwamba vitabu hivi vya mwishoni vya Agano Jipya vilithibitisha tena kwamba Ujio na Mwisho utatokea katika uhai wa waandishi wake, bali pia vinafundisha kwamba Ujio huo na Mwisho huo "uko karibu zaidi kutokea sasa kuliko wakati ule tulipoamini" (War. 13:11), na "uko mlangoni kabisa" (Yakobo 5:9; Ufunuo 3:20). Chati hii hapa chini inaonyesha jinsi hali ya ukaribu ilivyosababisha hisia kali jinsi mwaka 70 B.K. ulivyokaribia:

**3 KAULI ZA "YUKO KARIBU!" ZILIONGEZEKA MWISHONI**

| **Ubashiri wa *Mwanzo*** | **Kauli za *Baadaye* katika Agano Jipya** |
|---|---|
| Endeleeni kuwahubiria Waisraeli mpaka Kristo atakapokuja – Matt. 23; 24:14ff; 28:19-20 | Ondokeni Israeli, Ujio u karibu – Ufunuo 18:4; 22:6,7,10,12,20 |
| Mitume wote walikuwa hai wakati huo, lakini "baadhi" tu watakuwa hai hapo mwishoni – Matt. 16:27,28; Yoh. 21:22 | Ukweli wa kihistoria: wengi kati ya mitume walikuwa wamekufa kufikia 66 B.K. Yakobo alikufa 44 B.K. na wengine kadhaa katika kipindi cha 62 – 66 B.K. |
| Hakuwa "*mlangoni*" wakati huo, lakini itakuwa hivyo wakiona mambo hayo yakitokea – Matt. 24:33 | Walikuwa wakiyaona mambo yale yote yakitokea, hivyo sasa alikuwa "mlangoni" – Yakobo 5:9 |
| "*Dhiki Kuu*" itakuja wakati fulani katika kizazi hiki, chunguzeni nyakati mkitafuta ishara hizi ili mjue pale itakapokaribia – Matt. 24:21-31 | Dhiki Kuu ilikuwa ikitokea sasa: Matendo 11:19; 14:22; War. 5:3; 2Wakor. 1:8ff; 1Wathess. 1:6; 3:3; 2Wathess. 1:4-10; Ufu. 1:9; 7:14 |
| Yote yatatimia – Luka 21:22 wakati Israeli itakapopondwa-pondwa – Dan. 12:7 | Petro anarejea unabii wa wakati wa Agano la Kale na anatamka kwamba kutimizwa kwake kumekaribia 1Pet. 4:7 |
| Kifunge kitabu hiki – wakati wake uko mbali bado – Dan. 12:4,9 | Usikifunge kitabu hiki – wakati wake u karibu – Ufunuo 22:10 |
| Mbingu na nchi havitapita mpaka – Matt. 5:17,18; Matt. 24:29,35; Isa. 65,66 (mbingu & nchi) | Mbingu na nchi sasa viko tayari kupita – Waebr. 12:28; 2Pet. 3:13; Ufu. 21 (mbingu mpya na nchi mpya - Ufalme) |

| Ubashiri wa *Mwanzo* | Kauli za *Baadaye* katika Agano Jipya |
|---|---|
| Marejeo ya jumla kwa Majira yajayo –<br>Yoh. 6:44; 12:48; - Siku ya Mwisho<br>Matt. 24:3,6,14 – Mwisho wa Enzi unakuja<br>Matt. 24:34 – “Kizazi hiki”<br>Dan. 2:21; Matendo 1:7 – Nyakati na Enzi (pl) | Marejeo mahususi kuhusu ukaribu –<br>Siku imekaribia – Waebr. 10:25<br>Katika muda mfupi tu ujao – Waebr. 10:37<br>Saa ya mwisho – 1Yoh. 2:18<br>Wakati umefika, Muda mfupi sana – Ufu. 1:1-3; 22:10<br>Mwisho umekaribia – 1Pet. 4:7,17<br>Wakati wa hukumu – 1Pet. 4:17<br>Ujio umekaribia – Yakobo 5:8,9 |
| Uasi dhidi ya imani [yetu] utakuja – Waalimu, Manabii, Makristo wa uwongo – Matt. 24:10-14 | Uasi dhidi ya [imani] yetu umeanza – 1Yoh. 2:18; 2Wathess. 2:7; Yuda 18,19; 2Pet. 3:3 |
| Ukombozi bado haujakaribia – Lk 21:31;<br>Lk 19:11-27 | Ukombozi u karibu sasa – War. 8:23;<br>Waefe. 1:14; 4:30 |
| Ufalme utakuwa umekaribia watakapozion ishara hizi (Lk 21:31). Waturithi ufalme Bwana atakaporudi (Matt. 25:34) | Ufalme u karibu sana. Walikuwa wamekaribia kupokea urithi (Waebr. 12:28; Yak. 2:5;<br>2Pet. 1:11; Ufu. 11:15; 22:10) |
| Shetani na uzao wake watapondwa katika kizazi kile – Mwa. 3:15; Matt. 23:33; Yoh. 8:41-44 | Shetani atapondwa hivi karibuni! (Wae. 16:20; 1Pet. 5:1-10; Ufu. 22:6,7 |
| Siri na ukombozi utakamilishwa katika siku zile – Dan. 9:24; Dan. 12; Waefe. 1:9-14 | Siri na ukombozi sasa ulikuwa unakamilishwa – Ufu. 10:7; 12:10; Ufu. 21; Ufu. 22 |
| Miaka mingapi mpaka ule mwisho? Ni mpaka pale uweza wa watu watakatifu utakapovunjwa-vunjwa – Dan. 12:6-9 | Ni muda gani mpaka wafia-Kristo watakapothibitishwa? Itakuwa katika “muda mfupi tu ujao” – Ufu. 6:10,11; na Lk. 18:8 |
| Karamu ya harusi, atakapokuja bwana harusi – Matt. 22:2-13; 25:1-13 | Wakati wa karamu ya harusi umefika –<br>Ufu. 19:7-9 |
| Mavuno yatakuwa mwisho wa enzi – Matt. 13:30 | Saa ya mavuno imefika – Ufu. 14:15 |

Kama tunavyoona katika chati hapa juu, kauli zao za ukaribu ziliongezeka katika wingi wake na katika hisia kwa jinsi kizazi kile cha kwanza cha kanisa kilivyokuwa kinakaribia mwisho wake.

Albert Schweitzer na wengine waliponyooshea kidole mtanziko (dilemma) huu katika ukaribu wa mambo ya mwisho, baadhi ya wana-teolojia walijaribu kuepa kwa kusema kwamba maandiko ya mwanzo ya Agano Jipya yalipendekeza tu uwezekano wa ujio ulio karibu, lakini sio uhakika wa ujio huo. Halafu muda ulivyoenda na hali ya kuchelewa ilivyoonekana kuongezeka, waandishi wa baadaye wa Agano Jipya wakaanza kutoa dhana ya kuchelewa.

Lakini dhana hii inaenda kinyume na ukweli kama unavyoonekana. Muda ulivyoenda na vitabu vya mwishoni vya Agano Jipya vilipokuwa vinaandikwa, matarajio ya ukaribu wa Ujio hayakufifia hata kidogo, na badala yake hisia za matarajio ziliongezeka katika ukali wake. Maswali kama “Mpaka lini, Ee Bwana?” (Ufu. 6:10), na majibu kama “Katika muda mfupi sana” (Ufunuo 6:11; Waebr. 10:37; 1Pet. 5:10), yanaonyesha matarajio makubwa sana ya tukio linalongojewa. Kwa hakika, Petro aliwaambia wasomaji wake wa karne ya kwanza katika mwaka 63 B.K., mwaka mmoja tu kabla Wakristo hawajaanza kuteswa ya mfalme Nero, “muweke matumaini yenu kwa utimilifu katika ile neema mtakayoletewa wakati wa ufunuo wake Yesu Kristo” (1Pet. 1:13). Je, alikuwa

akiwapa matumaini ya uwongo ili baadaye awaone “wakianguka” ule Mwisho utakaposhindikana kutokea “katika muda mfupi ujao”? Hapana! Yesu alirejea punde tu, kama alivyoahidi.

Matukio yaliyomo katika kuharibiwa kwa Yerusalemu yanatoa muktadha timilifu wa kihistoria wa kurejea kwa Kristo. Hiyo ndiyo dondoo kuu ya Hotuba ya Mlima wa Mizeituni (Matt. 24 na sura zinazofanana katika zile Injili nyingine). Kuangamia kwa Yerusalemu katika mwaka 70 B.K. kulitokea ndani ya kizazi kile cha karne ya kwanza, na Ujio Wake ulihusiana moja kwa moja na hukumu ile juu ya Israeli. Kristo alirudi mwaka 70 B.K!

**4 JOSEPHUS NA HISTORIA YA KARNE YA KWANZA**

Kuna taarifa zenye mvuto mkubwa kuhusiana na maandiko ya Agano Jipya na maangamizi ya Yerusalemu katika maandishi ya kihistoria ya Josephus. Ingawa yeye si mwandishi aliyeongozwa na Mungu, lakini vitabu vyake vya historia vinaweza kuaminiwa kuwa na kiasi kikubwa cha usahihi. Yeye alikuwa kuhani wa Kiyahudi aliyetumikia katika hekalu, na alikuja kuwa mmoja kati ya majenerali wa juu kumi katika vita dhidi ya Rumi. Alikamatwa mapema sana katika vita ile, na kwa sababu ya utabiri wake kwamba Vespasian atakuwa mfalme wa Rumi, aliruhusiwa kusafiri na Warumi na kuandika kumbukumbu za vita. Sababu taarifa zake zina thamani (umuhimu) mkubwa ni kwamba yeye alikuwa shuhuda wa Kiyahudi, akiandika kwa ajili ya wasomaji wa Kirumi na wa Kiyahudi na hivyo alilazimika kuwa na usahihi mkubwa katika uandishi wake.

Josephus anasema kwamba kabla tu ya kuanza kwa vita majeshi ya malaika (“magari na vikosi vya askari … walipaa huku na kule mawinguni”) yalionekana yakiizunguka miji ya Kiyahudi, (Tazama ‘Kutimia Kulitajwa Katika Vitabu vya Josephus). Anaandika ukweli kwamba watu katika karne ya kwanza waliuita Yerusalemu “Mji Mkuu”, kama kitabu cha Ufunuo kinavyouita (Ufu. 11:8). Anasema kwamba vita ya mwaka 70 B.K. dhidi ya Rumi ilikuwa ni “Revolution of the Ages” – Mapinduzi ya Enzi (*pl*) – yaani mabadiliko kutoka enzi moja kwenda nyingine. Anazungumzia madimbwi ya damu na mioto mikubwa kama inavyosimuliwa katika Ufunuo 14:20 na aya nyingine. Je, Yesu hakubashiri kwamba mambo ya aina hii yatatokea (Luka 21:11, 25-27)?

Historia kama ilivyoandikwa na Josephus imetuwezesha kutambua mambo mengi katika hulka ya vita ile na umuhimu wake kwa Wayahudi na Wakristo. Lakini si Josephus peke yake aliyeandika mambo haya! Mwandishi wa historia wa Kirumi Tacitus, na mwandishi wa historia wa Kikristo Eusebius, wote wanasema mambo haya yalitokea! Na vitabu vya Talmud vinaandika mambo yanayofanana pia (Yoma, folio 39b). Baadhi ya maelezo bora ya ki-preterist yaliyomo katika maandishi ya mwanzoni ya wazee wa kanisa yanapatikana katika [vitabu vya] utetezi dhidi ya Wayahudi. Chilton amenukuu baadhi ya maelezo hayo katika kitabu chake Paradise Restored. Eusebius anampendekeza Josephus kuwa ni chanzo cha juu cha kuaminika cha taarifa kuhusu kuangamia kwa Yerusalemu (kwa jinsi Josephus anavyousimulia uharibifu ule), na anafikia hata kutamka, “… yote haya, nasema, yeyote mwenye shauku [ya kuyajua] anaweza kuyaona yameandikwa kwa usahihi [kabisa] katika historia iliyoandikwa na Josephus” (Book 3, chapter 5, Ecclesiastical History). Hapa chini kuna orodha ya dondoo [zilizobashiriwa katika Biblia] ambazo zilitimia, na kusimuliwa na Josephus.

Tunachomaanisha hapa ni kwamba matukio ya wakati wa mwisho yaliyobashiriwa yalitokea [vile vile yalivyobashiriwa, bila kukosa]. Tuna ushahidi wa Kibiblia na wa kihistoria. Waandishi wa Agano Jipya wanayasimulia matukio yale katika lugha ya ki-maafa, wakati Josephus, Tacitus, vitabu vya Talmud, na Eusebius wanasimulia kutimia kwa ubashiri ule wa Kibiblia katika lugha ya uhalisia wa matukio ya kila siku, ya wanadamu. Tunapaswa pia kuutazama uwezekano kwamba sababu kwa nini matukio ya Ujio wa Pili na Ufufuo wa Watakatifu haukusimuliwa na watu

walioyaona ni kwa sababu hawakuwa wanaishi hapa duniani baada ya matukio hayo. Wengi kati ya Wakristo halisi waliuawa katika mateso ya Nero, na waliobaki walibadilishwa na kuingia katika miili yao mipya isiyokufa na kupelekwa mbinguni na wanaishi huko na Kristo milele (1Thess. 4:15-17; Matt. 24:31; Yoh. 14:3).

**5 AINA 5 ZA KUTIMIA ZILIZOTAJWA KATIKA VITABU VYA JOSEPHUS**

1. Wayahudi wa kizazi kile walikuwa waovu kuliko wa kizazi kingine chochote cha kabla ya hapo – Matt. 12:45 (Wars 5:10:5) Ukiwalinganisha na Wasodoma (Wars 5:13:6).
2. Yesu alibashiri siku za kisasi, dhiki, na ghadhabu zitakuja juu ya Wayahudi. Josephus anazitaja "dhiki" hizi – Luka 21:20-24. (Wars 2:10:1; 2:22:1: 6:3:3,4; 6:9:2-4; 7:1:1).
3. Vita na Tetesi za Vita, Masihi wa Uwongo, na Manabii wa Uwongo walibashiriwa – Matt. 24:6; Matt. 24:6-26. (Antiquities 20:5:1-4; 20:8:5-10; Wars 2:10:1; 2:13:4-7; 2:17:8; 6:5:2 [6:285-288]).
4. "Ole" tatu zilizotamkwa dhidi ya Yerusalemu (Ufu. 8:13) – Josephus anamtaja nabii wa maangamizi aliyetumia maneno haya haya "ole" – (Wars 6:5:3 [6:300-309]).
5. Yerusalemu uliitwa "Sodoma" na "ule Mji Mkuu" Ufu. 11:8; 18:21-24; cf Lk 13:33-35 (Wars 5:13:6; 7:8:7).
6. Yerusalemu ulikuwa na biashara kubwa iliyoendeshwa kwa njia ya maji (bahari / merikebu), na ulikuwa "Capitol" – Bunge - juu ya wilaya kumi za Palestina – Ufu.17:12-17; 18:10-24 – (Wars Pref. Sec. 2.4; Wars 3:3:5; 7:1:1).
7. Wayahudi walipewa tahadhari [kabla] kwa ishara – Luka 21:25 – "maajabu yaliandamana na baadhi ya majanga makuu" (Wars 2:22:1-2; 4:4:5; 6:5:2-3).
8. Majeshi ya malaika yalionekana angani katika miji ya Kiyahudi (Matt. 24:30-31; 2Wathess. 1:7-8. Yuda 14; Ufu. 1:7 (Wars 6:5:3).
9. Sadaka za kuteketezwa (zilizokuwa zikitolewa kila siku) zilikoma "katikati ya wiki" (baada ya miaka 3 1/2) - Dan. 9:27 (Wars 6:2:1 tazama pia rejeo / tanbihi chini ya ukurasa ya Whiston kuhusu hii).
*10. Makundi matatu ya kijeshi yalianza kupigana wao kwa wao katika jiji la Yerusalemu (Eleazer, John na Simon), jambo ambalo liliwadhoofisha na kufanya iwe rahisi kwa Warumi kuwavamia na kuwashinda - Ufu. 16:19 (Wars 5:1:1-5)
*11. Wayahudi walipigana zaidi wao kwa wao kuliko walivyopigana dhidi ya Warumi na hivyo walijiletea madhara wenyewe kuliko madhara kutoka kwa Warumi! Cf Ezek. 38:21 (Wars 2:17:1-10; 2:18:1-11; 4:6:2,3; 5:1:2-5; 5:6:1; 5:13:6; 6:2:1).
*12. Wayahudi waliharibu miundombinu yao wenyewe ya kupata chakula na nyaraka za nasaba / koo na makabila (Wars 5:1:4 [5.24-25]; 6:6:3; [6.354]; 6:9:1)
*13. Mazingira ya kutisha na mabaya yalikuwako wakati Yerusalemu ilipozingirwa na majeshi ya Rumi. Njaa, tauni, mizoga na maiti zilizagaa kila mahala – Luka 19:43-44 (Wars 6:10:2; [5.425-7]; 6:8:1; 6:7:2; [6.369]; 6:9:3; [6.421]).
14. Madimbwi ya damu kama inavyosimuliwa katika Ufunuo 14:20; 17:16; Mat. 2:19 (Wars 2:18; [?]; 4:5:1; 5:1:2-5; 6:4:6; 6:5:1,2; 6:8:5).
15. Uasi wa Mazeloti ulikuwa kama "hayawani" wa porini anayekula nyama yake mwenyewe – Ufu.16:10; 17:16; 19:19-21 (Wars 4:7:4; 4:9:8; 5:1:1; 5:2:5).
*16. Ulaji wa nyama za watu – Walawi 26:29; Kumb. 28:53-57 (6:3:3-4). Njaa kali ilisababishwa na vita ya wenyewe kwa wenyewe kati ya makundi / madhehebu ya Wayahudi – Wars 5:1:4.
*17. "Mawe" ya 'mvua ya mawe' yenye uzito wa talanta moja – Ufu. 16:21 (Wars 3:7:9; 5:6;3).
18. Wayahudi ndio walioanza kuliunguza hekalu lao wenye, Warumi waliendeleza tu huo moto – Ufu. 17:16 (Wars 6:2:9; 6:3:5; 6:4:5; 6:6:2 [6.346].
19. Askari wa Kirumi walitoa dhabihu kwa bendera yao waliyoisimamisha ndani ya hekalu (Je, yaweza kuwa hili ndilo "Chukizo la Uharibifu"? - Matt. 24:15 (Wars 4:5:1; 5:1:2,3,5).
*20. Wayahudi waliuzwa kama watumwa – Lk 21:24 (Wars Pref. Sec. 11; 6:8:2; 6:9:2-4,17).

*21. Vyombo vya hekalu viliporwa na kupelekwa Roma na Titus (siyo yule Myahudi / Mkristo) {Wars 7:5:5-7}.
22. Halikubaki hata jiwe [moja] lililosimama juu ya jiwe – Matt. 24:2 (Wars 7:1:1 [7.1-3]; 7:8:7 [7.376-379]).
23. Dhiki ile ilikuwa kali zaidi ya zote milele – Yer. 30:7; Dan. 12:1; Matt. 24:21; Ufu. 16:18 (Wars Preface Section 4; Wars 5:10:5; 6:9:4 [6.429]).
24. Uharibifu wa mwaka 70 B.K. ulikuwa ndio tukio kuu la enzi zote [za wanadamu] – "mapinduzi ya enzi (pl)" na "mfumo wa dunia ulivurugwa" Matt. 24:3; 1Wakor. 7:29-31; 10:11; 1Yoh. 2:17:18 (Wars 4:4:5; 6:4:5).
25. Mungu (na si Warumi) ndiye aliyeuchukua ufalme kutoka kwa Wayahudi na kuupea kwa Kanisa Matt. 21:43 (Wars 6:8:4; 6:9:1,4).

* Soma orodha ya laana zinazotokana na kuvunja amri za Agano la Mungu: Walawi. 26:14-39; Kumb. 28:15-68.

## 6 JOSEPHUS ANATAJA *'SIKU NA SAA'*

Katika hotuba ya Mlima wa Mizeituni (Matt. 24 na sura zinazofanana katiki zile Injili zingine), Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba watakapoona ishara fulani, hapo watajua kwamba Ujio Wake umekaribia:

24:33Vivyo hivyo nanyi, myaonapo haya yote, basi mjue ya kuwa yu karibu, tena milangoni.
24:34Amin, nawaambieni, Kizazi hiki hakitapita, bila haya yote kutimia.
24:35Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita.
24:36Lakini juu ya siku ile na saa ile hakuna ajuaye, hata malaika walio mbinguni, ila Baba yangu pekee.
25:13Basi kesheni, maana hamwijui siku wala saa atakayokuja Mwana wa Adamu.
Matt. 24:33-36; 25:13 (Tafsiri kutoka KJB)

Yesu hakuwapa siku wala saa mahususi atakayorudi, lakini aliahidi kwamba kurejea kwake kutatokea katika kizazi kile kabla watu wote waliokuwa hai wakati ule hawajafa. Na aliwapa ishara zitakazowaongoza, zitakazowaonyesha pale ujio wake utakapokaribia. Alimwambia hata Petro kwamba hautatokea mpaka atakapokuwa mzee na kuuawa (Yoh. 21:18).

Lakini Josephus, akiandika baada ya matukio yale, anataja siku na saa ambayo majeshi ya malaika yalionekana angani yakiashiria ujio wa Yesu [kwa ajili] ya kuwafufua wafu kutoka kuzimu (Hades), kuwaokoa watakatifu wake walio hai kutoka katika Dhiki Kuu waliyokuwa wakipitia, na kumwaga ghadhabu yake juu ya watesi wao:

> Siku kadhaa baada karamu ile (Pasaka 66 B.K.), siku ya 21 ya mwezi Artemisius (Iyar), mwujiza mkuu wa kushangaza ulitokea; nadhani masimulizi ya mwujiza huu yataonekana kama hekaya, ikiwa hayatasimuliwa na wale walioushuhudia, na ikiwa matukio yaliyofuata yasingekuwa na umuhimu mkubwa kiasi cha kustahili sifa zile; kwani, **kabla ya saa ya machweo**, *magari na vikosi vya askari walionekana wakikimbizana mawinguni, na wakizunguka miji*. Zaidi ya hayo, katika ile karamu [nyingine] inayoitwa siku ya Pentecost, wakati makuhani walipokuwa wakiingia katika ukumbi wa ndani wa hekalu saa ya usiku, kama ilivyokuwa desturi yao, ili wakatimize huduma zao takatifu, walisema kwamba, kwanza *walihisi tetemeko [la ardhi], na wakasikia sauti kuu, na baada ya hapo wakasikia sauti kama ya kundi kubwa la watu, wakisema, "Ebu sisi tuondoke hapa!*" [Whiston, Complete Works of Josephus, Wars 6:5:3 (6.296-300).

Majeshi ya malaika [kwanza] yalionekana angani kabla tu ya machweo katika siku ya 21 ya mwezi wa Artemis (April mwaka 66), kitu kilichoashiria mwanzo wa Ujio wa Kristo kwa ajili ya kutoa thawabu na kuhukumu. Chini ya miezi miwili baadaye (June 66 B.K.), jioni ya siku ya Pentecost, [wakati] makuhani walipokuwa wakiingia hekaluni kutimiza majukumu yao ya kawaida, walisikia sauti kuu na ya watu wengi sana ikitoka katika himaya isiyoonekana, ikisema, "Ebu sisi tuondoke hapa!" Hili kwa dhahiri lilikuwa tukio la ufufuo wa watakatifu kutoka kuzimu (Hades). Hivyo, bila kujua, Josephus alitupatia siku yenyewe na saa ya mwanzo wa Ujio (Parousia), pamoja na *siku na saa* ya ufufuo wa wafu. Alitupa uthibitisho wa ubashiri wa Yesu kuwa ni wa kweli hadi *"siku na saa"* ya tukio lenyewe, katika kizazi kile kile, "kabla baadhi ya waliokuwa wakisimama pale" hawajaonja mauti.

**7 UJIO "MDOGO TU" MWAKA 70 B.K.?**

Kuna wengi wanaoamini kwamba kulikuwa na "aina fulani ya ujio wa Kristo" kuhusiana na kuangamia kwa Yerusalemu katika mwaka 70 B.K., lakini pia wanaongezea kwa haraka sana kwamba ulikuwa ujio "mdogo" tu wa Yesu, na kwamba ujio "mkubwa" wa Yesu bado uko katika siku zetu za usoni! Wanauita "*ujio katika hukumu dhidi ya taifa la Kiyahudi.*" Hata hivyo, swali ni kwamba, "Ni sehemu gani katika Agano Jipya [ambapo] panatofautishwa kati ya ujio mdogo katika hukumu na ujio mkubwa wa Kristo?" Si Yesu mwenyewe wala waandishi wa Agano Jipya wanatafuta muda wa kutueleza ni "ujio" upi wanaouzungumzia. Hakuna hata mmoja wao anayesema "**Hapa** namaanisha ujio mdogo tu wenye lengo la kuumaliza ulimwengu wa Kiyahudi, lakini **pale** nitazungumzia *ujio mkubwa* kwa ajili ya kuumaliza ulimwengu mzima."

Ebu mfikirie Mkristo wa karne ya kwanza aliyeishi kabla ya kuangamia kwa Yerusalemu mwaka 70 B.K. ambaye alikuwa na nakala za nyaraka chache tu za Agano Jipya. Je, Mkristo huyu angeweza kujua kwamba Yesu alikuwa anazungumzia "ujio wa Mwana wa Adamu" utakaotokea *mara mbili tofauti* utakaotenganishwa na miaka elfu kadhaa kati ya ule wa kwanza na wa pili? Sisi [ Wakristo wa leo] tuna wakati mgumu katika kupambanua "ujio" mbalimbali unaotajwa, nasi tunaishi miaka 2000 baada ya 70 B.K., na tuna vitabu vyote vya Agano Jipya! Agano Jipya halifundishi "ujio" wa Kristo zaidi ya mmoja. Alikuwa anarudi mara moja tu, na ujio huo ulitokea katika karne ya kwanza wakati wa maangamizi ya Yerusalemu. Anawezaje *kurudi tena* kama *hakuondoka tena*? Alikuja katika karne ya kwanza (70 B.K.). Bado yuko nasi. Hataondoka. Siku zote atakuwa nasi.

Waumini wa Kanuni za Imani (Creedalists) hawakubaliani na dhana ya kuuweka Ujio wa Pili wa Kristo katika miaka ya nyuma. Hata hivyo baadhi yao wanaamini kwamba kulikuwa na aina fulani ya ujio "mdogo" katika mwaka 70 B.K., na patakuwa na ujio "wa mwisho" katika siku za usoni. Dhana ya ujio huu wa mara nyingi ni shambulizi kali zaidi dhidi ya Kanuni za Imani kuliko madai yetu [sisi preterists] kwamba Kristo alirudi mara moja tu mwaka 70 B.K. na si siku za usoni, kama zinavyodai Kanuni za Imani. Kanuni [za Imani] zinazungumzia ujio [wa pili] mmoja tu. *Partial Preterists, ambao wanaongeza Ujio wa Tatu utakaotokea [wakati wa] mwisho wa ulimwengu, ujio ambao haukubaliani na orodha ya matukio ya siku za mwisho katika Kanuni za Imani (Creeds), wamekiuka Kanuni hizo kwa kiasi kikubwa zaidi ya **Full Preterists ambao wametafsiri tu upya majira ya Ujio wa Pili unaotajwa katika Kanuni za Imani na Maandiko. Ni nani anayekiuka zaidi mafundisho ya Kanuni za Imani? Wale wanaotafsiri upya majira ya Ujio wa Pili, au wale

*Partial Preterism ni tafsiri ya Eskatolojia inayofundisha kwamba kuna matukio ya mwisho wa ulimwengu ambayo hayajatimia bado, na yatatimia katika Ujio wa Pili wa Kristo utakaotokea siku za usoni.
**Full Preterism ni tafsiri ya Eskatolojia inayofundisha kwamba matukio yote ya siku za mwisho (kiyama) yamekwishatokea.

wanaoongeza Ujio mwingine katika orodha?

Sote tunapaswa kutambua kwamba Kanuni za Imani zinaweza kuwa na makosa, na zinapaswa kusahihishwa pale zinapoonekana kuwa na kosa. Dhana hii inatia hofu katika mioyo ya Creedalists (Wakristo wanaoamini Kanuni za Imani) kwa sababu tu hawatambui kwamba wao wenyewe wamekiuka Kanuni [hizi]. Baadhi ya *Futurists na Partial Preterists wanasumbuliwa na kuukataa msemo "alishuka kuzimu" (descent into Hades) katika Kanuni ya Athanas na Kanuni ya Mitume, licha ya ukweli kwamba msemo huu una msingi imara katika Maandiko (Zaburi, Matendo 2 na 1Petro) na historia ya mwanzo kabisa ya kanisa. Tena Athanasius anasema kuhusu dondoo zote katika Kanuni yake (pamoja na dondoo ya "kushuka / alishuka") kwamba, "Hii ndiyo Imani **Katoliki: ambayo ikiwa mwanadamu hataiamini kikamilifu, [basi] hataokolewa". Sasa hii inawaweka wapi wale Creedalists ambao pia ni Partial Preterists wanaoikataa dondoo ya "Alishuka kuzimu"?

Waprotestanti wote wanaozungumza Kiingereza wanaghani tafsiri za Kiingereza za Kanuni za Mitume na Nicea ambazo zimebadilishwa. Katika lugha zake asilia za Kilatini na Kiyunani, kanuni hizi zimeandika "resurrection of the **flesh**" – ufufuo wa mwili / nyama. Lakini Reformers hawakulipenda neno *flesh* – nyama / mwili – hivyo wakatumia neno **body – *kiwiliwili*** – mahala pake katika tafsiri za Kiingereza.

*Swali*: Je, Reformers pekee ndio walikuwa na haki ya kubadilisha maneno katika Kanuni hizi? Au kila kizazi cha Wakristo kina uhuru wa kutokubaliana na baadhi ya maneno, na kuyasahihisha kama makosa yataonekana? Wino ulikuwa hata haujakauka katika Kanuni asilia ya Nicea kabla watu hawajaanza kujadili mabadiliko katika maneno fulani. Kanuni hizi hazina kikwazo kwa mtazamo wa ki-preterist kwa sababu [hizi] ni nyaraka za kibinadamu tu na hazina mamlaka ya Mungu kama Biblia. *Biblia pekee* ndiyo yenye mamlaka ya mwisho katika masuala ya kanuni. Na kama Maandiko [yaliyotoka kwa Mungu] yanafundisha mtazamo wa ki-preterist, haijalishi ikiwa Kanuni ambazo ni maandiko ya wanadama zinasimama dhidi yake. Jambo pekee la muhimu ni, Je, Maandiko yanafundisha mtazamo huu? Kanuni za wanadamu haziwezi kupinga mtazamo unaotokana na Maandiko yaliyotafsiriwa na kueleweka kwa usahihi.

## 8 TAREHE YA UANDISHI WA KITABU CHA UFUNUO

Tafsiri sahihi ya vitabu vingi vya Biblia aghalabu haitegemei wala kuathiriwa na tarehe ya uandishi wake. Lakini katika kukielewa kitabu cha ufunuo, tarehe ya uandishi wake ni muhimu sana. Tafsiri ya kitabu hiki inaathiriwa moja kwa moja na ufahamu sahihi wa tarehe ya uandushi wake. Kama kitabu hiki kiliandikwa kabla ya kuangamia kwa Yerusalemu, basi kuna shaka ndogo sana ya kwamba kitabu hiki kinahusiana na tukio hilo. Lakini kama kitabu hiki kiliandikwa miaka kadhaa baada ya mwaka 70 B.K., basi haiwezekani kuwa kilikuwa kimeandikwa kuhusiana na tukio la uharibifu wa Yerusalemu, kwani hiki ni kitabu cha unabii unaozungumzia kiasi kikubwa cha uharibifu katika muda mfupi uliofuata. Uchunguzi wa tarehe ya uandishi wa kitabu cha Ufunuo unaofanywa kwa uangalifu hautashindwa kutazama kazi ya Dr. Kenneth Gentry (*Before Jerusalem Fell*), David Chilton (*Days of Vengeance*), Foy Wallace (*The Book of Revelation*), and Arthur Ogden (*The Avenging of Apostles and Prophets*).

Baadhi ya watu wanaweka tarehe ya uandishi wa kitabu cha Ufunuo kuwa ni 96 B.K., msingi wake ukitegemea zaidi katika ushuhuda unaozaa maswali mengi wa mapokeo ya wazee wa kanisa la

*Futurist ni mtu anayeamini kwamba Ujio wa Pili [na Kiyama] bado viko katika siku za usoni.
**Neno Katoliki / *Catholic* maana yake ni '_ya mahala pote na wakati wote'.

mwanzo kabisa. Katika ushuhuda wake wa ndani, kitabu cha Ufunuo kinathibitisha ukaribu wa kurejea kwa Kristo na matukio mengine ya wakati wa mwisho. Tazama kwa makini Ufunuo 1:1,3 na 22:6,10. Aya hizi zinasema kwamba masimulizi ya kitabu hiki (unabii) yalikaribia kutimizwa punde tu. Masimulizi yale yanasema kwamba "mambo haya yanapaswa kutokea punde" kwa sababu "wakati" wa kutimizwa kwake "ulikuwa umekaribia." Moja kati ya matukio yaliyobashiriwa kutokea "punde" lilikuwa ni kurejea kwa Kristo ("kwa hakika ninakuja punde" Ufu. 22:7, 12,20). Kama kitabu hiki kiliandikwa mwaka 96 B.K. kama ambavyo watu fulani wanadhani, basi wanalazimika kutafuta tukio fulani kuu lililotokea punde baada ya mwaka 96 B.K. ambalo lina umuhimu wa kutosha kusababisha liitwe "Ujio wa Pili" na kutimizwa kwa unabii wa Ufunuo! Ufalme wa Rumi ulianguka baada ya miaka 300 iliyofuata! Mateso ya Warumi dhidi ya Wakristo hayakuisha katika mwaka 96 B.K., na kwa hakika hayakuisha mpaka karne mbili na nusu baadaye! Hakuna tukio kuu lililotokea punde baada ya 96 B.K. Je, inawezekana 96 B.K. si tarehe sahihi ya uandishi wa kitabu cha Ufunuo? Je, yaweza kuwa 70 B.K ndiyo tarehe sahihi? Ufunuo ni kitabu kinachojadili tukio la 70 B.K., tukio ambalo ni muhimu sana kiasi kwamba Biblia haikuweza kulifumbia macho na kuzungumzia mambo mengine yenye umuhimu mdogo sana (kama kifo cha Domitian).

Na kwa mtazamo wa Kiyahudi, ingekuwa ni ajabu sana kwamba Mungu aliwaangamiza watu Wake bila hata ya kitabu kimoja cha unabii kuzungumzia tukio hilo! Tukio lenye umuhimu mdogo zaidi la uvamizi na uharibifu wa Babeli dhidi ya Yerusalemu la mwaka 586 K.K. lilibashiriwa na vitabu vingi vya unabii (kabla, wakati, na baada ya tukio), na lugha inayotumika kulizungumzia tukio hili inafanana sana na lugha ya kitabu cha Ufunuo. Kabla Mungu hajawachukulia watu Wake hatua za kinidhamu, mara zote alinyanyua manabii ili wawatahadharishe watu wake hao juu ya toba, haswa kama kutakuwa na uharibifu mkubwa (kama ule wa 70 B.K.)! Na mara zote aliwapa vitabu vya unabii kuhusiana na uharibifu husika. Haiingii akilini kabisa kwamba Mungu atatoa unabii kwa utondoti [mkuu] kuhusu kuanguka kwa ufalme fulani wa kipagani (Rumi), na asitoe unabii wa aina yoyote kuhusu kuangamia kwa kishindo kwa taifa lililoasi [dhidi Yake] la Israeli katika 70 B.K! Kitabu cha Ufunuo kwa hakika kinaonekana kuwa ni hicho tunachokizungumzia.

Wale wanaokitafsiri kitabu cha ufunuo kwa kukihusisha tu na [mfalme] Domitian na ufalme wake wa Rumi wanasahau kile ambacho kitabu kinatudhihirishia. Kitabu cha Ufunuo hakizungumzii tu kifo cha "mnyama", lakini pia kinasimulia juu ya kuanguka na kuangamia kwa "Mji Mkuu Babeli" na mwisho wa mateso yaliyokuwa tishio haswa. Wale wanaofikiri kitabu hiki kinamzungumzia Domitian na Rumi wanasahau matukio haya mawili [ya historia]. Na hawawezi kutueleza jinsi ufalme wa Rumi na mateso ya Wakristo yalivyoisha punde baada ya mwaka 96 B.K! Kwa hakika hapakuwa na matukio ya aina hiyo punde baada ya mwaka 96 B.K. Ufalme wa Rumi ulikuja kuanguka miaka 300 baadaye, na mateso ya Warumi dhidi ya Wakristo yaliisha katika siku za mfalme Constantine, mwaka 313 B.K! Huwezi kusema kwamba matukio haya mawili yalitokea "punde" baada ya 96 B.K! Itakuwa inawazungumzia Wazelote na mateso ya Wayahudi dhidi ya Wakristo ambayo yaliisha punde tu katika mwaka 70 B.K. Mji gani "Mkuu" ulio muhimu kwa Wakristo na Wayahudi ulianguka "punde" baada ya mwaka 96 B.K? Mateso gani makuu yaliyokuwa tishio kubwa kwa kanisa yaliisha "punde" baada ya mwaka 96 B.K? Hakuna! Ufunuo 11:8 inalitambulisha lile "Jiji Kuu" ni lipi ("aliposulibiwa Bwana wetu"): Yerusalemu! Ufunuo 18:24 pia inatutambulishia ule "Mji Mkuu" ni upi: "*Na ndani yake ilionekana damu ya manabii na ya watakatifu na ya wale wote waliouawa juu ya inchi*." [Petro, katika 1Pet. 5:13, anasema, "***Kanisa katika Babeli***, lililochaguliwa pamoja nanyi linatuma salamu kwenu ..."]

Haya yote yanapolinganishwa na tamko la Bwana Yesu katika Matt. 23:29-39 na Luka 13:33-35, unaweza kuona kwamba "Jiji Kuu" linalotajwa katika kitabu cha Ufunuo ni Yerusalemu, na si Roma! Yesu anasema kwamba Yerusalemu ndio mji "unaoua mitume," na kwamba "hatia ya damu

yote ya haki iliyomwagika juu ya nchi" itauangukia Yerusalemu katika kizazi kile (Matt. 23:34-37). Utakapolinganisha kauli hizi za Yesu na Ufunuo 18:24, hitimisho lake haliepukiki: Yerusalemu ndilo "Jiji Kuu"! Na kama kitabu cha Ufunuo kinazungumzia kuanguka kwa Yerusalemu, basi kiliandikwa kabla ya mwaka 70 B.K. ili kiweze kubashiri kuanguka kwake.

Mateso gani makuu yanazungumzwa katika kitabu cha Ufunuo? Vitabu vingine vya Agano Jipya vinataja mateso makubwa ambayo Wayahudi waliyafanya dhidi ya Wakristo (Matt. 10:16-23; Matt. 24:9,10,21; Matendo 8:1; Waga. 1:13; etc). Mateso haya dhidi ya Wakristo yalikoma mwaka 70 B.K! Kifo cha Domitian mwaka 96 B.K. hakikukomesha mateso ya Warumi dhidi ya Wakristo. Eusebius alisema mateso ya Warumi dhidi ya Wakristo yaliendelea kwa karne mbili zilizofuata. Mateso yale hayakuisha "punde" baada ya mwaka 96B.K! Lakini kama kitabu kiliandikwa muda mfupi kabla ya mwaka 70 B.K., basi palikuwa na kikomo cha mateso makubwa "punde" baada ya hapo.

Katika Matt. 23:32-37, Yesu anasema kwamba Wayahudi wa kizazi kile ndio waliokuwa tishio halisi kwa Wakristo. Ilikuwa ni Wayahudi (na si Warumi) ambao damu iliyomwagwa ya wenye haki itahesabiwa juu yao. Uongozi mbovu wa Wayahudi wa kizazi kile ndio waliowatesa Wakristo "kutoka mji hadi mji." Mji wa Yerusalemu ndio ambao hatia ya damu ya mitume na watakatifu ilihesabiwa juu yake. Kitabu cha Matendo ya Mitume kinadhihirisha kwamba sababu pekee Warumi walihusika katika mateso dhidi ya Wakristo ilikuwa kwamba Wayahudi walihitaji kupata kibali kupitia [mamlaka ya] watawala wa Kirumi ili waweze kutimiza vitisho vyao.

Wayahudi wasiokuwa waaminifu kwa Bwana Yesu ndio walikuwa tishio dhidi ya wafuasi wa Kristo. Hata Paulo anasema, katika Waga. 1:13,23; 1Tim. 1:13; Matendo 8:3; 9:21, kwamba nia yake kama mtesi wa Wakristo kabla hajawa Mkristo haikuwa kujadiliana nao ili kuwathibitishia kwamba walikua katika makosa. Alikuwa anajaribu "kuwaangamiza!" Wakati wote ambapo viongozi wa Kiyahudi wa kizazi kile walikuwa na madaraka basi walikuwa tishio kwa Wakristo. Hakuna watu waliojua "namna na mbinu" za kuwaangamiza Wakristo zaidi ya Wayahudi. Mfumo wa ibada za hekalu wa Kiyahudi ulikuwa unapata changamoto kubwa kutoka kwa Wakristo, na viongozi wao walihisi kufedheheshwa! Kwa kipindi walichokuwa na madaraka (mpaka 70 B.K.), walifanya kila walichoweza kuuondoa Ukristo kabla haujaota mizizi.

Baada ya 70 B.K., mateso na manyanyaso yalikuwepo, lakini hayakuwa katika kiwango cha kutishia uwepo wa Wakristo kama mateso ya Wayahudi yalivyokuwa. Eusebius (Book II, chapter 25 na Book III, chapters 5-8), anaonyesha kwamba mateso kutoka kwa Wayahudi yalikuwa tishio kali kweli. Palikuwa na jamii za Kiyahudi zilizoenea kote katika ufalme wa Rumi, na Wayahudi waliobadilika na kuwa Wakristo katika siku ile ya Pentekoste ya kwanza walirudi makwao wakiwa na Injili. Haikuchukua muda mrefu kwa Wakristo hao kuonyesha uwepo wao na kuutangaza utofauti wao [mpya]. Mateso makali yalianza mara moja dhidi yao. Barua za Paulo na kitabu cha Matendo vinaonyesha mgogoro huu uliokuwa ukiendelea wakati wote. Hali ilikuwa mbaya muda ulivyokuwa ukiendelea.

Ilipofahamika kwamba watu wa Mataifa wanaweza kuokolewa bila ya tohara [ya wanaume], bila kutimiza Sheria ya Musa, na kwamba dhabihu za hekaluni hazikuhitajika tena wala hazikupokelewa tena na Mungu, viongozi wa Wayahudi walishikwa na ghadhabu kuu. Hawakuruhusu kitu chochote kiwazuie katika juhudi zao za kukomesha "kufuru" hii mpya. Mihimili yao yote ya imani ilikuwa ikikanyagwa na Wakristo hawa! Na pale mfalme Nero wa Rumi alipohusishwa, mateso dhidi ya Wakristo yakaenea katika himaya yote [ya Kirumi], na kwa haraka sana mateso yale yalifikia kiwango cha kuitwa "dhiki kuu" ambamo mitume kadhaa waliuawa na wengine kufungwa.

Josephus anatupatia tarehe ya kuanza kwa "dhiki kuu" kuwa ni mwaka 62 B.K. baada ya kifo cha Festus na Ananus II akasimikwa kama kuhani mkuu. Uyahudi ilikuwa bila gavana wa Kirumi kwa miezi mitatu. Ananus II akaichukulia hii kama fursa ya "kumkamata Yakobo na baadhi ya washirika wake." Ilikuwa ni katika miaka hii minne ya "dhiki kuu" (takriban 62 – 66 B.K.) ndipo Yakobo, Paulo na Petro waliuawa, na mtume Yohana akafungwa katika kisiwa cha Patmos, alikoandika kitabu cha Ufunuo. Katika sura ya ufunguzi ya kitabu cha Ufunuo, Yohana anaandika, "Mimi Yohana, ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na ustahamilivu ulio katika Yesu Kristo, nilikuwa katika kisiwa kiitwacho Patmos, kwa sababu ya Neno la Mungu, na kwa sababu ya ushuhuda [wangu] juu ya Yesu." Mwandishi Mkristo wa historia Papias aliyeishi mwishoni mwa karne ya kwanza aliandika kwamba Yohana aliachiwa kutoka Patmos na akaishi Efeso, ambako aliuawa na Wayahudi katika kipindi cha mateso ya Nero ("dhiki kuu").

Mtume Petro, aliyeandika wakati huu (63 – 64 B.K.), anasema kwamba Shetani alikuwa amefunguliwa, na alikuwa "akizungukazunguka, akitafuta mtu wa kumla" (1Pet. 5:8). Petro alijua kwamba kifo chake cha ushuhuda kimekaribia (2Pet. 1:14) kwa sababu Shetani alikuwa amefunguliwa na dhiki kuu ilikuwa ikiendelea. "Dhiki" hii ilianza kwa Wakristo (1Pet. 4:17), na mara moja Aliudhika na akashuka na malaika Wake mwaka 66 B.K. na kuanza kumwaga ghadhabu na hukumu juu ya taifa la Kiyahudi kwa miaka mitatu na nusu (66 – 70 B.K.).

Katika Matt. 24:22,42 Yesu anasema kwamba kama "dhiki" ile haitakatishwa, hakuna hata "mteule" atakayebaki kumlaki siku Atakaporudi! Tukio la uasi wa Wayahudi lilikatisha dhiki ile. Wayahudi walilazimika kugeuzia akili na nguvu zao katika vita dhidi ya Warumi. Kuangamia kwa Yerusalemu katika mwaka 70 B.K. kuliwadhoofisha Wayahudi kwa kiasi kukubwa hivyo hawakuwa tena tishio dhidi ya Wakristo. Walilazimika kujishughulisha na kutunza uhai wao wenyewe, na ikumbukwe, Mungu alikwishawatelekeza. Na kuharibika kwa hekalu mwaka 70 B.K. kulisimamisha kabisa shughuli za kutoa dhabihu. Hii ilikuwa ishara kwa wote kwamba Ukristo ndio ulikuwa imani halali.

Kitabu cha Ufunuo kiliahidi ahueni ya haraka kwa wahanga wa dhiki kuu ile, na ilikuja haraka sana. Mateso ya Nero [dhidi ya Wakristo] yalianza katika Kiangazi cha mwaka 64 B.K., na yakakatizwa na kufumuka kwa uasi wa wayahudi [dhidi ya Rumi] wa mwaka 66 B.K. Hii inaoana na uanbii wa Ufunuo kwa utimilifu mkubwa, na hivyo tunajua kwamba kitabu cha Ufunuo kiliandikwa kabla ya dhiki kuu, bila shaka katika Kiangazi cha mwaka 62 B.K. Kukipa kitabu hiki tarehe ya uandishi wake kuwa ni 96 B.K. kumekuwa ndiyo sababu kubwa kwa nini imekuwa vigumu kukielewa kitabu hiki. Kinakuwa kitabu rahisi kutafsiri mara unapong'amua kwamba kiliandikwa kabla ya 70 B.K.

**9 TAREHE YA KITABU CHA UFUNUO KABLA YA 70 B.K.**

Hapa chini kuna orodha ndefu ya wafasiri wa Biblia walioweka tarehe ya uandishi wa kitabu cha Ufunuo kuwa ni kabla ya 70 B.K. katika uandishi wao. Ni bayana kwamba tarehe hii inakubalika na wanazuoni wengi. Kenneth L. Gentry, Philip Schaff, F. W. Farrar, John A. T. Robinson, E. P. Gould, Milton S. Terry na wengine (katika vitabu vyao vinavyoorodheshwa katika bibliografia ya kitabu hiki unachokisoma) wanawataja zaidi ya wana-teolojia mia moja katika kipindi cha karne 4 zilizopita ambao wameweka tarehe ya uandishi wa Ufunuo kuwa ni kabla ya 70 B.K. Kati ya hawa, K. L. Gentry (Before Jerusalem Fell, ukurasa wa 30 na kurasa zinazofuata) amekuwa na msaada mkubwa sana [katika kutoa ushahidi wa kisomi]. Wengine kati ya wana-teolojia hawa pia wanaamini katika kutimia (kabla ya 70 B.K.) kwa ubashiri wote au mwingi wa kitabu cha Ufunuo. Na hawa si watu wasiofahamika au wasio na umaarufu! Wengi wao wamo katika "Who's Who" ya wanazuoni wa Biblia. Walioorodheshwa katika hati nzito hapa chini wanapendekezwa mahususi kwako kwa mafunzo yako ya ziada. Vingi kati ya vitabu vyao vimo katika bibliografia. Baadhi ya vitabu vyao vipo, au vinapatikana mtandaoni katika tovuti mbalimbali.

Andreas (karne ya 5), Arethas (karne ya 10), Theophylact (1071), Luis De Alcasar (1554-1613), Henry Hammond (1653), **John Lightfoot** (1658), Hugo Grotius (1664), Sir Isaac Newton (1727), **Frank Abauzit** (1733), Hardouin (1741), **J. J. Wettstein** (1751), Bishop Thomas Newton (1754), Harenburg (1759), **Johann Gottfried Von Herder** (1779), **E. G. Hartwig** (1780), Eichorn (1791), **N. Nisbet**t (1802), J. C.L. Gieseler (c. 1820), Frederick Bleek (1820), F. H. A. Ewald (1828), F. J. Züllig (1834), **J. A. Stephenson** (1838), **Moses Stuart** (1845), Albert Schwegler (1846), Wm. M. L. Dewette (1848), Gottfried Friedrich Lücke (1852), Karl A. Auberlen (1857), Düsterdieck (1859), Charles **Pettit M'llvaine** (1859), **F. D. Maurice** (1861), **Philip S. Desprez** (1861), **Charles Wordsworth** (1866), **J. B. Lightfoot** (1867), **B. Weiss** (1869), **Henry Cowles** (1871), **James Glasgow** (1872), H. Gebhardt (1873), J. E. Renan (1873), A. Hilgenfeld (1875), A. Immer (1877), Dean Plumptre (1877), **James M. McDonald** (1877), **James Stuart Russell** (1878), **Robert Young** (1822-1888), **Israel P. Warren** (1878), **Alexander Brown**, **R. W. Dale** (1878), J**. T. Harris**, J. H. Noyes, **Thomas Rattray** (1878), Edward Reuss (1880), Samuel Davidson (1882), **B. F. Westcott** (1882), **Milton S. Terry** (1883), **William Hurte** (1884), August Neander (1889), **F. W. Farrar, C. A. Goodhart** (1891), A. Plummer (1891), T. Randell (1891), W. H. Simcox (1893), W. Sanday (1893), **F. J. A. Hort** (1894), **William Newton Clarke** (1894), E. Hampden Cook (1894), G. O. Field (1895), **John David Michaelis,** Philip Schaff, E. P. Gould (1896), G. Salmon Dean Stanley Tilloch, F. C. Baur, Aube, Krenkel, Reville, Volkmar, Bunsen, Rudolf Stier, Guericke, Niermeyer, Hentenius, Edward Robinson, Dr. Dollinger, E. C. Selwyn (1900), **William S. Urmy** (1900), B. W. Henderson (1903), H. J. Holtzman (1912), G. Edmundson (1913), A. S. Peake (1919), A. Weigall (1930), A. D. Momigliano (1934), Ulrich Beeson (1956), C. C. Torrey (1958), K. A. Eckhardt (1961), James Hamilton (1962), Jay Adams (1966), **Foy Wallace** (1966), Max R. King (1971), Franklin Camp (1974), J. Massyngberde Ford (1975), Ray Hawk, John A.T. Robinson (1976), Jessie E. Mills, Jr. (1978), Edward E. Stevens (1978), Cornelius Vanderwaal (1979), Burton Coffman (1979), Timothy A. James (1982), David H. Chilton (1985)**, Arthur M. Ogden** (1985), Greg L. Bahnsen (1989), **Kenneth L. Gentry, Jr**. (1989), Ron McRay (1990), Janice E. Leonard (1991), John Noe (1991), Joseph R. Balyeat (1991), Kenneth J. Davies (1992), **Don Preston** (1992), Gary DeMar (1994), **Albert R. Pigeon** (1994), Eugene Fadeley (1995), Joseph M. Daniels (1996), John L. Bray (1996), **Arthur Melanson** (1998), Robert Charles Sproul (1998), Daniel E. Harden (1999), Randall E. Otto (2000), James A. Henry (2002), Samuel M. Frost (2002), **Tom and Steve Kloske** (2003), Kurt M. Simmons (2003), **Brian L. Martin** (2004)**, Ian D. Harding** (2005), **Michael Alan Nichols** (2010), Glenn L. Hill (2010), Stephen Temple (2012), Tony Everett Denton (2012), Charles S. Meeks (2013), na idadi inayoongezeka kila siku ya wengine wengi. Inaelekea kwamba takriban mwanzoni mwa karne ya 21 (2001 B.K.), waandishi na uandishi wenye mtazamo wa ki-preterist ulianza kuongezeka kwa kiasi kikubwa, na hakuna dalili kwamba kasi yake itapungua hivi karibuni. [Wakristo wameanza kuutazama unabii katika macho mapya.]

## 10 NABII DANIELI NA UFUNUO

Nabii Danieli aliahidiwa kwamba kutakuwa na ufunuo zaidi kuhusiana na "mambo haya" utakaotolewa "katika wakati / majira ya mwisho" (siyo "mwisho wa wakati / majira" – kuna tofauti kubwa!) wakati watu wake watakapokuwa "wamevunjwa-vunjwa kabisa" (Dan. 12:4-9). Kuvunjwa-vunjwa kamili kwa Wayahudi tangu majira ya Danieli mpaka leo kulitokea katika maangamizi ya 70 B.K! Hivyo basi, "majira ya mwisho" yanayozungumzwa katika Danieli 12 ni lazima yalikuwa ya kizazi cha 70 B.K. Kirai kinachotumiwa na Danieli ni "majira ya mwisho", na si "mwisho wa majira". Kuna tofauti. Hakuna mahala katika Biblia

panapofundisha kurejea kwa Kristo katika “mwisho wa majira.” Futurists wamefanya mengi tu katika kutatanisha wasomaji wa mambo haya. Bwana Yesu na wanafunzi wake wanarejea unabii wa Danieli, na wanautumia kufasili matukio ya karne ya kwanza na mwaka 70 B.K. “Wakati wa mwisho” wa Danieli ni “mwisho kamili” utakaotokea pale Wayahudi “watakapovunjwa-vunjwa kabisa (tazama Dan. 9:26,27; 10:14; 11:27,35,40; 12:4,6,7,9,13). Ulikuwa ni “wakati huo huo wa mwisho” ambapo “chukizo la uharibifu” lilijulikana na kuangamizwa. Danieli aliambiwa “kukifunga” kitabu chake kwa sababu “wakati wa mwisho” ulikuwa bado mbali sana katika siku za usoni [mwake] (Dan. 12:4,9). Lakini, Yohana aliambiwa asikifunge kitabu chake cha Ufunuo kwa sababu wakati wa kutimizwa kwake “ulikuwa karibu” (Ufu. 22:10). Watu wengi wana muafaka kwamba Ufunuo inazungumzia jambo lile lile kama Danieli, hivyo basi kitabu cha Ufunuo kitakuwa kinahusu ufunuo ule wa ziada unaohusiana na “kuvunjwa-vunjwa kabisa” kwa Wayahudi kulikofunuliwa kwa Danieli. Hii ina maana kwamba kizazi ambacho Ufunuo kiliandikwa ni lazima kilikuwa kile cha “wakati wa mwisho.” Na tukilinganisha wasifu wa malaika (Dan. 10:5,6; Rev. 1:13-15) aliyewapa Danieli na Yohana ufunuo huu, tunaona kufanana kwa kiasi kikubwa sana, jambo linalopendekeza tena ukweli kwamba kitabu cha Ufunuo kwa hakika ni mwendelezo wa ufunuo ulioahidiwa kutolewa katika “majira ya mwisho.”

Danieli anazungumzia “wakati wa mwisho” wa taifa la Uyahudi ambapo watu wake “watavunjwa-vunjwa kabisa” (Dan. 12). Hivyo kama kitabu cha Ufunuo kinazungumzia mambo yale yale kama kitabu cha Danieli, basi nacho kitakuwa kinazungumzia mambo ya 70 B.K. pia. Na kama kitabu cha Ufunuo kina ujumbe kuhusu mwaka 70 B.K. basi kiliandikwa kabla ya mwaka huo ili kiweze kubashiri matukio yake.

Wakati anabashiri nyakati za uharibifu zitakazowafikia Wayahudi mwaka 70 B.K., Yesu alisema, “… Hizi ni siku za kisasi, ili yote yaliyoandikwa yapate kutimizwa” (Luka 21:22). Hapo anaonyesha kwamba unabii wote wa Agano la Kale utatimia utakapofika wakati wa kuangamia kwa Yerusalemu. Hii ina maana kitabu cha Danieli, ambacho ni unabii wa Agano la Kale, kitatimia kufikia mwaka 70 B.K.

## 11 MATTHAYO 24 NA UJIO WA PILI

Matt. 24 na aya zinazofanana katika Injili nyingine (Marko 13; Luka 17; and Luka 21), zinatupatia ushahidi wa nguvu kwamba Yesu alirudi mwaka 70 B.K. Ukianza katika Matt. 23:29 na kuendelea moja kwa moja mpaka mwisho wa sura ya 24, ni lazima utaona ukaribu wa matukio yanayosimuliwa pale. Katika Matt. 23:36, Yesu anasema, “*Mambo haya yote yatakuja juu ya kizazi hiki.*” Anaongeza katika Matt. 24:34, “*Kizazi hiki hakitapita, bila haya yote kutimia.*” Tazama kwa makini, anasema, “mambo haya yote”, na si baadhi yake tu! Na moja kati ya “mambo” yanayotajwa katika muktadha huu ni “*kuja kwa Mwana wa Adamu*” (Matt. 24:3, 27, 30, 37, 39, 42, 44, 46, 50)! Hivyo, ama Yesu alirejea katika kizazi kile (ndani ya takriban miaka 40, tazama Waebr. 3:10-17), au Yeye na waandishi wa Agano Jipya walikosea (na hawakuongozwa na Mungu).

Baadhi wanajaribu kuepa mtanziko huu kwa kuigawanya Matthayo 24 katika sehemu mbili, ya kwanza ikijadili mwaka 70 B.K. (aya ya 1-34), na ya pili ikijadili mwisho wa ulimwengu katika siku za usoni [mwetu] (aya ya 35 na aya zinazofuata). Chati hii hapa chini (Hotuba ya Mlima wa Mizeituni Haiwezi Kugawanywa) inaonyesha kwa nini mtazamo huo hauwezi kuwa sahihi.

## 12 KUHUSIANA NA JEDWALI

Tazama jedwali hapa chini. Baadhi wana msimamo unaoonekana upande wa kushoto wa jedwali hili. Wanafikiri kwamba Matt. 24 inazungumzia vipindi 2 tofauti vya majira:

1. Sehemu A – Matukio Yanayohusika na Mwaka 70 B.K.
2. Sehemu B – Matukio Yaliyo Siku za Usoni Mwetu.

Wanayaweka matukio yote yanayotajwa katika Matt. 24:1-34 (Sehemu A) katika kipindi cha kwanza cha wakati (70 B.K.), na matukio yanayotajwa katika Matt. 24:35ff wanayaweka katika siku za usoni [mwetu].

Lakini, maelezo ya Luka katika sura ya 17 (upande wa kulia wa jedwali) yanatuonyesha kwamba dhana hii haiwezi kuwa sahihi. Luka 17 inajadili matukio yale yale kama Matthayo 24, lakini bila hata kudokeza kwamba vipindi hivi viwili tofauti vimo akilini mwake. Ni wazi kabisa kwamba Luka anayachukulia matukio haya yote kwamba yanatokea katika kipindi kimoja (“siku atakayofunuliwa Mwana wa Adamu,” Luka 17:30).

**13. KUTOGAWANYIKA KWA HOTUBA YA MLIMA WA MIZEITUNI**

| Matt. 24 | Luka 17:20-37 |
|---|---|
| Sehemu A (Matukio yanayohusishwa na 70 B.K.) | Yote ni Sehemu moja (mwaka 70 B.K.) |
| 1. Aya za 17,18 - "… Naye aliye juu ya nyumba asishuke avichukue vitu vilivyomo nyumbani mwake …" | 2. Aya za 23-24 - " Kwa maana kama vile umeme [wa radi] umulikavyo toka upande huu …" |
| 2. Aya za 26,27 - "… Kwa maana kama vile umeme [wa radi] utokavyo mashariki …" | 4. Aya za 26,27 - " Na kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika siku za Mwana wa Adamu" |
| 3. Aya ya 28 - "… Maana popote mzoga utakapokuwapo, ndipo [hapo] tai watakapokusanyika ..." | 1. Aya ya 31 - "Katika siku ile, aliye juu ya nyumba, na vyombo vyake ndani ya nyumba, asishuke ili kuvitwaa: naye aliye shambani vivyo hivyo asirejee nyumbani." |
| Sehemu B (Matukio yaliyo katika siku za usoni?) | |
| Matt. 24:35 na aya zinazofuata | |
| 4. Aya ya 37 - "Lakini kama vile ilivyokuwa [katika] siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu" | 5. Aya za 35,36 - " Wanawake wawili watakuwa wakisaga pamoja, mmoja atatwaliwa, na mmoja ataachwa" |
| 5. Aya za 40,41 - "Wakati huo watu wawili watakuwa shambani; mmoja atachukuliwa, mmoja ataachwa … " | 3. Aya ya 37 - " Wakajibu wakamwambia, Wapi, Bwana? Akawaambia, Mzoga uliko ndiko watakakokusanyika tai." |

**Muhtasari wa Hapo Juu:**

| A | |
|---|---|
| 1. Juu ya Nyumba | 2. Umeme / Radi |
| 2. Umeme (Radi) | 4. Nuhu |
| 3. Mzoga | 1. Juu ya Nyumba |
| B | |
| 4. Nuhu | 5. Kusaga / Shambani |
| 5. Kusaga / Shambani | 3. Mzoga |

Tazama katika jedwali hapo juu jinsi Luka anavyoorodhesha matukio yale yale kama Matthayo, lakini katika mpangilio tofauti. Mpangilio katika Matthayo ni 1,2,3,4,5, lakini mpangilio wa matukio yale yale katika Luka umewekwa katika orodha tofauti ya 2,4,1,5,3! Luka ameorodhesha tukio kutoka Sehemu A (Umeme / Radi) likifuatiwa na tukio kutoka Sehemu B (Nuhu), halafu ana tukio kutoka Sehamu A (Juu ya Nyumba) likufuatiwa na tukio kutoka Sehemu B (Kusaga / Shambani). Hii inatuletea tatizo: Kama ni kweli Matt. 24 ina sehemu 2 (au vipindi 2 tofauti vya majira) vinavyojadiliwa, basi maelezo ya Luka si sahihi, kwa sababu anachanganya (‘anavuruga’) matukio haya matano kama vile yote yatatukia katika kipindi kimoja cha majira / wakati. Ama Luka amekosea (na hivyo Injili yake haijatoka kwa Mungu), au ni makosa kugawanya matukio yaliyomo katika Matt. 24 katika sehemu 2. Hata hivyo, ufumbuzi wa mgogoro huu ni kwamba Matthayo na Luka wanazungumzia matukio yale yale ambayo yanatokea katika kipindi cha wakati ule ule. Na katika Matt. 24:34 tunaambiwa kipindi hicho cha wakati ni kipi: “kizazi” kilichokuwa hai wakati Bwana Yesu anatamka maneno hayo (30 – 70 B.K.).

“Ujio” ule ule “wa Mwana wa Adamu” unajadiliwa katika zile zinazodaiwa kuwa ni sehemu mbili (Matt. 24:3, 27, 30, 37, 39, 42, 44, 46, 50 – tazama maneno ya Kiyunani yanayomaanisha “kuja / ujio”). Sura hii haiwezi kugawanywa katika ujio wa aina / mara nyingi. Matukio yote katika “Sehemu” zote mbili yameunganishwa na “Ujio” ule ule “wa Mwana wa Adamu.” Sehemu ya pili ina aina ile ile ya aya za “Ujio” kama Sehemu ya kwanza, ikitumia maneno / misamiati ile ile ya Kiyunani (***parousia*** na ***erchomai***) inayomaanisha Üjio.” Neno la Kiyunani “parousia” linatumiwa mara nne, mara mbili katika kila Sehemu. Tumeziorodhesha hapa chini kwa ajili ya urahisi wa kulinganisha. Soma aya husika za Biblia ili uone mwenyewe kama kuna dalili yoyote inayoonyesha kwamba Yesu alikuwa anazungumzia “Ujio” wa aina mbili tofauti “wa Mwana wa Adamu” unaotenganishwa na miaka elfu kadhaa.

**1. Sehemu ya Kwanza – (Matt. 24:4-34) –** Ujio wa 70 B.K.

• “parousia” – Matt. 24:3, 27
• “erchomai” – Matt. 24:30
**2. Sehemu ya Pili – (Matt. 24:35ff) –** Ujio Unaodaiwa Kutokea Siku za Usoni
• “parousia” – Matt. 24:37, 39

• “erchomai” – Matt. 24:42, 44, 46, 50

Wafasiri wengine (kw. mf Marcellus Kik, Ken Gentry) wanadai aya zote zinazotaja “Ujio” katika Sehemu ya Kwanza zinahusiana na 70 B.K., na wanaendelea kusema kwamba aya zote za “Ujio” zilizo katika Sehemu ya Pili zinahusika na “Ujio katika Utukufu” utakaotokea siku za usoni. Kutofautisha sehemu hizo mbili kusikokuwa na mantiki wakati aya za sehemu zenyewe zinatumia maneno yale yale ya Kiyunani kumewafungulia mlango wakosoaji (kama Bertrand Russell, Albert Schweitzer, na wengine wengi) wa kumshutumu Yesu kuwa amekosea. Kutenganisha sura ya 24 kunamaanisha kwamba Yesu alikuwa anazungumzia matukio mawili ya Ujio yanayotenganishwa na maelfu ya miaka (linganisha Matt. 24:27 na Matt. 24:37,39) akitumia si tu “lugha inayofanana”, bali akitumia lugha na kirai kile kile (“Ujio wa Mwana wa Adamu). Neno “Parousia” (kuja / ujio) linatumika katika sehemu zote mbili, na matukio yanayotajwa katika sehemu zote mbili yanahusiana na parousia hiyo ya Mwana wa Adamu. Ama tunalazimika kusema kwamba matukio yote haya yako katika siku zetu za usoni (na kumfanya Yesu kuwa ni mwongo kwa kusema kwamba hayo yote yatatokea katika kizazi kile), au tuseme kwamba yote yalitimia katika mwaka 70 B.K. Preterists ndio pekee wana hoja thabiti, zinazokubaliana katika suala hili.

Yesu mwenyewe kamwe hatofautishi kati ya “kuja” mara mbili “kwa Mwana wa Adamu” akifuatana na “malaika wake katika utukufu” pamoja na “mawingu.” Tungelazimika kupata

ubainisho wa suala hili mahala pengine katika mafundisho Yake, kwani haupatikani katika muktadha wa Matt. 24. Kumbuka pia kwamba neno “parousia” halitumiwi na Yesu mahala pengine popote katika Injili zile nne. Linatumika hapa tu katika Matt. 24, na linatumika kimbadala na neno lingine linalotafsiriwa “kuja / ujio”, *erchomai*. “Parousia” na “erchomai” ni maneno yanayotumika kimbadala, yaani kwa maana ile ile katika muktadha huu mahala pote penye mjadala wa “ujio wa Mwana wa Adamu.” Hivyo hakuna mahala katika mafundisho ya Yesu ambapo anatofautisha kati ya “parousia” mbili tofauti zinazotenganishwa na miaka elfu kadhaa. Ni wazi kabisa kwamba watakatifu wa karne ya kwanza hawakuwa na uelewa wa parousia mbili hapa. Waliujua ujio [wa Pili] mmoja tu wa Kristo.

Waandishi wa Agano Jipya pia hawakuandika kuhusu parousia mbili zinazotenganishwa na maelfu ya miaka. J. N. D. Kelly, Jaroslav Pelikan, Kurt Aland, T. F. Torrance na wanazuoni wengine wengi waangalifu wa historia ya Kanisa wamesisitiza jinsi kanisa la kabla ya mwaka 70 B.K. lilivyoenea na kusheheni mafundisho ya ukaribu wa parousia moja. Albert Schweitzer amedhihirisha jinsi ukaribu wa parousia moja ndio ulikuwa “uzi uliofuma kitambaa” cha Agano Jipya.

Ukweli kwamba palikuwa na parousia moja tu, na kwamba ingetokea katika kizazi kile, unawapa *mtanziko usioshindikana kwa ‘Futurists’, na unawaacha wakiwa rahisi kushambuliwa na waliberali na ma-skeptics (Watia-shaka) ambao wanadai kwamba kwa hakika Yesu aliahidi kurejea mara hiyo moja tu na katika kizazi chake Mwenyewe, lakini alishindwa kutimiza ahadi hiyo. Kwa kuwa Futurists hawaamini kwamba Ujio huo ulitokea kweli katika kizazi kile, basi inawalazimu kumchukulia Yesu kuwa ni nabii wa uwongo. Mtazamo wa Ki-preterist sio tu unatoa nadharia bora zaidi kuhusu mtanziko wao huu, bali unatoa ufumbuzi *pekee* wa mtanziko wenyewe. *Mtanziko – dilemma.

Tunapoitafakari Matt. 24, tunapaswa kutazama kwa makini Matt. 24:14, ambapo Yesu anasema, “Na injili hii ya ufalme itahubiriwa katika nchi yote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; ndipo ule mwisho utakapokuja.” Hili ni moja kati ya yale matukio yaliyomo katika “Sehemu A” ya Matt. 24 (tazama jedwali, juu), ambalo lazima lilitimizwa kabla ya 70 B.K. Je, kuna uthibitisho wowote kwamba lilitimia? Ndiyo, tazama War. 1:8; 10:18; 16:26; Wakol. 1:6, 23. Baadhi ya aya hizi zinatumia maneno na virai vile vile vinavyotumika katika Matt. 24:14. “Mwisho” (Matt. 24:14) lazima ulitokea!

Tunapaswa kuona jinsi sura hizi tatu (Matt. 23,24,25) zinavyounganishwa katika muktadha wake. Huu si mkusanyiko wa matamshi kuhusu matukio yasiyo na uhusiano wowote kati yao. Hotuba hizi zilitolewa katika siku moja, na zinazungumzia somo moja ambalo Bwana Yesu alilianzisha katika Matt. 23 (ujio wa Mwana wa Adamu unaoambatana na majanga na uharibifu juu ya Yerusalemu). Hii inaanza kuonekana pale zile kauli za “Sehemu B” katika jedwali letu (hapo juu) zinapochunguzwa. Tazama katika Matt. 24:40,41 (yaani, “mmoja atachukuliwa, mmoja ataachwa”) Kuna kauli zinazofanana katika Luka 17. Ili mtu awaye yote asifikirie kwamba huu ni unyakuo, tunahitaji tu kusoma Luka 17:37 kuondoa shaka yoyote. Pale wanafunzi wanamwuliza Yesu “ni wapi” watu hawa watapelekwa. Watapelekwa mahala ambapo mizoga hupelekwa na kuliwa na tumbusi. Aya hizi zinabashiri kwamba kutakuwa na watu watakaopona uharibifu huu na ambao wataachwa nchini baada yake. Kama aya hizi zingekuwa zinazungumzia mwisho wa ulimwengu, pasingebakia mtu yoyote. Hivyo aya hizi zinazungumzia uharibifu wa Yerusalemu.

Kuhusiana na unyakuo, Preterists wameonyesha kwamba lugha inayotuymika hapa katika Matt. 23 - 25 ina angalau mifanano 15 na lugha inayotumika katika 1Wathess. 4 na 5. Mifanano muhimu kati ya hii inapatikana katika Matt. 24:29-31, ambapo panazungumzia kukusanywa kwa watakatifu na malaika. Kukusanywa huku, au “unyakuo”, kulitokea mwaka 66 B.K. kabla tu ya Vita ya Wayahudi.

Watu wachache sana wanatilia shaka uhusiano kati ya Matt. 23 na Matt. 24. Lakini umoja kati ya sura ya 24 na 25 umewekewa alama ya kuuliza. Matt. 25:1-13 ni mfano wa wale bikira kumi. Mfano huu unazungumzia kurejea kwa Bwana Harusi (Kristo). Katika Matt. 25:14-30, Yesu anafundisha kwa mfano mwingine unaoitwa Mfano wa Talanta. Mfano huu nao unahusiana na "kurejea" kwa Bwana. Mwisho, katika Matt. 25:31-46, Yesu anazungumzia "hapo atakapokuja Mwana wa Adamu." Mtu anawezaje kuamini kwamba "kuja" kote huku kwa Mwana wa Adamu kunakotajwa katika sehemu hizi zote tatu za Matt. 25 kunazungumzia "kuja" tofauti na kule "kuja" kunakozungumziwa katika sura ya 24? Kama kusingekuwa na kauli za "kuja" katika sura ya 25, tungeweza kuwa na uhalali wa kutilia shaka umoja wa sura zote tatu. Lakini sura zote tatu zinazungumzia kuhusu "ujio wa Mwana wa Adamu" bila ya kutofautisha katika "kuja" huko. Si Yesu wala waandishi wa Agano Jipya wanatofautisha kati ya matukio mawili ya kurejea kwa Kristo ambayo yanatenganishwa na maelfu ya miaka. Kutokuwako kwa tofauti katika Agano Jipya kwa ujumla, na mahususi hapa katika Matt. 23-25, kunalazimu tuone kwamba sura hizi tatu zina umoja, na zinazungumzia kurejea kwa Kristo katika mwaka 70 B.K.

Inaweza kutusaidia kuona, wakati tunajadili wakati wa tukio lile moja pekee la parousia (ujio) wa Kristo katika karne ya kwanza, kwamba neno "parousia" lilikuwa neno lililotumika na wanazuoni wa Kiyunani katika kuzungumzia ziara ya mfalme katika eneo moja kati ya maeneo mengi ya nchi anayoitawala. Ilikuwa ni ziara ya muda mrefu, wakati mwingine ikichukua hata zaidi ya mwaka, ili kutoa thawabu kwa raia wake waaminifu, na kuwaadhibu raia waasi. Hii inaonekana kuwa ndiyo dhana inayojadiliwa hapa kuhusu ujio wa Kristo. Halikuwa tu tukio la siku moja au la "kufumba na kufumbua." Lilikuwa tukio la kuwapa thawabu wanafunzi Wake waliokuwa waaminifu na kumwaga ghadhabu yake juu ya Wayahudi ambayo ilianza mwaka 66 B.K. na kuendelea angalau mpaka Yerusalemu ilipoangamizwa mwaka 70 B.K.

**14 VITABU VYOTE VYA AGANO JIPYA VILIANDIKWA KABLA YA 70 B.K.**

Tumeona kwamba kitabu cha Ufunuo kiliandikwa kabla ya kuharibiwa kwa Yerusalemu, na tunapotumia vigezo vya ushahidi wa ndani [ya kitabu chenyewe] na ule wa kihistoria katika kutathmini tarehe ya uandishi wake, vitabu vingine vyote vya Agano Jipya vinaonekana kuwa viliandikwa kabla ya mwaka 70 B.K. pia. Hata hivyo, hakuna ushahidi wa kihistoria unaoweza kusemwa kwamba unaaminika kwa asilimia 100 katika kutathmini tarehe ya uandishi wa vitabu hivi kuwa ni kabla au baada ya mwaka 70 B.K. Katika kutathmini tarehe ya uandishi wa vitabu vya Biblia, ushahidi wa ndani unaotolewa na Mungu mwenyewe siku zote ndio wa kuaminika zaidi.

Dr. John A. T. Robinson, mwana-teolojia anayejulikana sana kwa kuwa "m-liberali", aliushitua ulimwengu wa wanazuoni pale alipopendekeza kwamba vitabu vyote vya Agano Jipya viliandikwa kabla ya mwaka 70 B.K. Kwa kawaida, huu ni msimamo wa wanazuoni wa "conservative" – watu wasiopenda mabadiliko [ya haraka] – kwani wanazuoni wengi wa ki-liberali wanasimama katika tarehe ya baada ya mwaka 70 B.K. kama tarehe ya uandishi wa vitabu vingi vya Agano Jipya. Dr. Robinson anasema yeye alianza utafiti wa kitabu chake pale alipoona kwamba hakuna hata kitabu kimoja cha Agano Jipya kinachotaja tukio la kuharibiwa kwa Yerusalemu kama tukio lililopita. Yeye anasema kuharibiwa kwa Yerusalemu ni "tukio pekee ambalo tarehe ya kutokea kwake inajulikana kuliko matukio yote mengine katika karne ya kwanza, na pia ndilo tukio kuu la karne hiyo", na kila mara anatilia mkazo dondoo / dhana kwamba tukio muhimu kama hilo lisingeweza kupuuzwa na waandishi wa Agano Jipya kama lingekuwa limekwishatokea wakati wanaandika vitabu vyao. Katika kitabu chake, *Redating the Book of Revelation*, uk. wa 13, "Moja kati ya mambo yanayoshangaza sana kuhusu Agano Jipya ni kwamba … kuanguka kwa Yerusalemu katika mwaka 70 B.K. … hakutajwi hata mara moja kama tulikio lililokwishapita". Yawezekana vipi kwamba hakuna hata mwandishi mmoja wa Agano Jipya anayeshangazwa na usahihi wa ajabu wa ubashiri wa Bwana Yesu kuhusu

kuharibiwa kwa Yerusalemu katika Matt. 24? Hata kama hawakuwa na ushuhuda wa moja kwa moja wa uharibifu ule, angalau kungekuwa na aya fulani chache zinazozungumzia maisha baada ya kuharibiwa kwa hekalu na jiji la Yerusalemu ambazo zingetuonyesha ufahamu wao wa tukio hilo, na hivyo kutuonyesha kwamba walikuwa wanaandika baada ya mwaka 70 B.K. Dr. Robinson anasema kwamba kukosekana kwa vidokezo vya matukio ya 70 B.K. katika vitabu vya waandishi wa Agano Jipya ni jambo lenye umuhimu “kama kutobweka kwa mbwa kulivyokuwa muhimu kwa Sherlock Holmes” (uk. 13). Waandishi wa Agano Jipya hawakuyataja matukio ya 70 B.K. kwa sababu wakati wanaandika yalikuwa hayajatokea bado! Vitabu vyote vya Agano Jipya viliandikwa kabla ya 70 B.K.

Kwa kuwa unabii (kunena / kuandika) kwa kuongozwa na Mungu ilikuwa ni moja kati ya karama za Roho Mtakatifu, kufungwa kwa [uandishi wa vitabu vya ziada vya] Biblia katika mwaka 70 B.K. kunalazimu kutufahamisha kwamba karama ya unabii (ufunuo) ulikoma wakati huo pia. Vitabu kadhaa vimeandikwa vikifundisha [dhana] kwamba karama ya unabii (ufunuo) ilisitishwa mwaka 70 B.K. J. S. Russell, Cornelius Vanderwaal, George E. Gardiner, Franklin Camp, Guy N. Woods, and Don Preston ni baadhi tu ya waandishi hao. Hii inatupatia tarehe ya wazi kabisa ya kukamilishwa kwa uandishi wa vitabu vya Agano Jipya.

Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba karama zote za Roho Mtakatifu zimesitishwa. Kuna Preterists wakarismatiki wanaokubaliana kwamba vitabu vyote vya Agano Jipya viliandikwa kabla ya mwaka 70 B.K., lakini wanaendelea kushikilia msimamo kwamba baadhi au vipawa / karama zote nyingine zilibakia na zinaendelea. Kwa bahati njema, kuendelea au kusitishwa kwa karismata si jambo la msingi. Hivyo Preterists na Futurists wanaweza kutofautiana katika suala hili bila kuvuruga ushirika wao.

Tunapaswa kukumbuka kwamba siku zote Mungu amekuwa akiwatunza na kuwalea watu Wake. Biblia haifundishi kwamba matunzo na malezi Yake yatasitishwa. Vinginevyo, tutalazimika kuacha kuomba kwa Mungu kwa ajili ya kuwaponya wagonjwa. Baadhi ya makusudi na kazi za Roho Mtakatifu kama Paraklete (Mfariji) wakati wa kipindi cha mpito yalikuwa ni ufunuo wa unabii, kuthibitisha / kutia nguvu na kukamilisha ili kulijenga Kanisa (Yoh. 14:26; 15:26; 16:8-15; 1 Cor. 1:8; Eph. 4:11-16; Heb. 2:3). Tazama kwa makini alichokisema Bwana Yesu kuhusu kazi ya Paraklete (John 14:26; 15:26; 16:8-15):

> “Atawafundisha mambo yote”
>
> “Atawakumbusha yote niliyosema kwenu”
>
> “Atatoa ushuhuda juu Yangu, nanyi mtanishuhudia”
>
> “atauthibitishia ulimwengu kuhusu dhambi, haki na hukumu”
>
> “atawaongoza katika kweli yote”
>
> “atawafunulia yote yajayo”

Huu ni ufunuo, uthibitisho na ukamilisho kuhusiana na kukamilisha wokovu. Tunapaswa kufahamu kwamba kazi hizi za Paraklete (kuwawezesha mitume kufundisha na kuandika kwa ufunuo) zimemalizika, labda kama tunataka kudai kwamba kuna kanuni za kweli za ziada zitakazofunuliwa. Yuda 3 na Ufunuo 22:18-19 ni aya ambazo haziachi nafasi yoyote kwa ajili ya dhana ya kuendelea kwa ufunuo baada ya uandishi wa vitabu vya Agano Jipya kumalizika:

Wapenzi, nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia kuhusu wokovu wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia, ili niwasisitize muipiganie imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu. Yuda 3 (Tafsiri kutoka BSB)

22:18 Nashuhudia kwa kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii katika kitabu hiki: Mtu yeyote akiongeza mengine, Mungu atamwongezea mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki.
22:19 Na mtu yeyote akiondoa baadhi ya maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.

22:20 Yeye mwenye kuyashuhudia haya asema, Naam; Nakuja punde. Amina: na uje Bwana Yesu!

Ufunuo 22:18-20 (Tafsiri kutoka BSB)

Ufunuo wa Maandiko umesitishwa. Paraklete alimaliza kazi Yake ya ufunuo kuhusu mpango wa ukombozi kuelekea wakati Yerusalemu inaangamizwa mwaka 70 B.K.

## 15 JE, BADO TUMO KATIKA SIKU ZA MWISHO?

Wakristo wengi leo wanafikiri kwamba bado tupo katika "siku za mwisho." Lakini katika Matendo 2:16-20, Petro anaeleza kwa wazi kwamba "Siku za Mwisho" zilikuwa zinaendelea (Waebr. 1:1-2), na kwamba siku hizo za mwisho zitafika mwisho wake katika ile Siku Kuu na ya Kutisha ya Bwana. Kirai "Siku ya Bwana" ambacho Petro na waandishi wengine wananukuu, ni msemo unaotumika mara nyingi katika vitabu vya mitume wa Agano la Kale [katika] kuelezea uharibifu / kuangamia kwa taifa fulani ovu (tazama Isa. 13:6-19; Isa. 24-34; Isa. 51,52; Yer. 4; Ezek. 30:1-12; Ezek. 32; kitabu chote cha Yoeli, haswa 1:15–2:11; Hag. 2; Zef. 1:7-14; Zak. 14; nk). Kirai / msemo huu HAUZUNGUMZII mwisho wa dunia.

Aya hizi "zina-sound" kama mwisho wa ulimwengu, lakini muktadha wake unadhihirisha kwamba zinazungumzia tu kuanguka kwa mataifa husika. Ulikuwa ni "mwisho wa ulimwengu" kwa mataifa hayo ovu. Katika muktadha wa Matendo 2:16-20, Petro anaashiria kwamba "Siku hizo za Mwisho" ziliwahusu Wayahudi aliokuwa anawahubiria. Katika Matendo 2:40, anawasisitiza kutubu na [hivyo] "kujiokoa wenyewe kutoka kizazi hiki potovu" kilichoandikiwa maangamizi. Hapo inakuwa wazi na rahisi kuelewa kwamba misemo "Siku za Mwisho" na "Siku Kuu na ya Kutisha ya Bwana" ilikuwa inamaanisha kizazi kile cha mwisho cha Wayahudi walioishi kabla ya kuangamia kwa Yerusalemu.

Mwaka 70 B.K. Yesu alirejea na kuzimaliza siku za mwisho za taifa la Wayahudi. Ilikuwa Siku Kuu na Tukufu ya Mungu kwa ajili ya kuwahalalisha watu Wake na Siku ya Kutisha ya Hukumu na Uharibifu kwa wale waliomkana na kumsulubu na kuwatesa wafuasi Wake. Matendo 2:16-20 ni aya [za unabii] zilizotimia mwaka 70 B.K. Siku za mwisho za taifa la Kiyahudi ziliisha hapo. Ufalme mpya wa Milele ulianza hapo. Sisi hatuishi katika "Siku za Mwisho", wala "Siku Kuu na ya Kutisha ya Bwana" haiko mbele yetu (siku za usoni). Sasa tumo katika Ufalme wa Milele!

## 16 JE, UFALME WA MILELE ULISHAKUJA?

Ndani ya Ukristo, kuna uwanda mpana wa mafundisho kuhusu *hulka* ya Ufalme wa Milele, pamoja na wakati ufalme huo ulipotakiwa kuja / kuanza. Aya za maandiko zinazonukuliwa hapa chini zinaonyesha kwamba Ufalme ulitakiwa kufika katika majira ya kizazi cha "baadhi ya wale waliokuwa wamesimama pale" wakimsikiliza Yesu anafundisha. [Ufalme huu] ulitakiwa kuwa na hulka ya kiroho na wa kudumu milele.

***Wakati wa kufika kwa ufalme huu:***

Dan. 2:44 Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele.

Marko 1:15 [Yahana Mbatizaji] akinena, Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia…

Matt. 4:17 Tokea wakati huo Yesu akaanza kuhubiri, na kusema, Tubuni: maana ufalme wa mbinguni umekaribia.

Marko 9:1 AKAWAAMBIA, Amin, nawaambieni, Kuna watu katika hawa waliosimama hapa ambao hawataonja mauti hata watakapokuwa wameuona ufalme wa Mungu ukija kwa enzi.

Matt. 25:31 Siku atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake: 25:32 Na mataifa yote watakusanyika mbele yake: naye atawatenganisha kama vile mchungaji anavyotenganisha kondoo na mbuzi: 25:33 Atawaweka kondoo mkono wake wa kuume, lakini mbuzi mkono wake wa kushoto. 25:34 Kisha Mfalme atawaambia wale walio mkono wake wa kuume, Njoni, enyi mliobarikiwa na Baba yangu, mrithi ufalme mliotayarishiwa tangu ilipowekwa misingi ya ulimwengu:

Marko 21:31 Nanyi vivyo hivyo, mtakapoona hayo yakitokea, tambueni ya kuwa ufalme wa Mungu u karibu kabisa.

***Hulka ya Kiroho:***

Yohana 3:3 Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.

Matt. 18:1 WAKATI ule ule wanafunzi wakamwendea Yesu wakiuliza, Ni nani basi aliye mkuu kafika ufalme wa mbinguni? 18:2 Yesu akamwita mtoto mdogo, akamweka katikati yao, 18:3 Akasema, Amin, nawaambieni, Msipoongoka na kuwa kama watoto, hamtaingia kabisa katika ufalme wa mbinguni. 18:4 Basi, ye yote anyenyekeaye kama mtoto huyu [mdogo], huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni.

Luka 17:20 Na alipoulizwa na Mafarisayo, lini ufalme wa Mungu utakapokuja, akawajibu, akasema, Ufalme wa Mungu hautaonekana kwa macho. 17:21 Wala watu hawatasema, Tazama, uko huko au huku! Kwa maana, ufalme wa Mungu umo kati yenu.

Yohana 15:19; 17:14 – Katika ulimwengu, lakini si wa ulimwengu.

Yohana 18:36 - Yesu akajibu, Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu, kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu: watumishi wangu wangalinipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi: lakini sasa ufalme wangu sio wa hapa.

Matt. 5:3Wamebarikiwa walio masikini wa roho: maana ufalme wa mbinguni ni wao.

Marko 9:35 Akaketi, akawaita wale thenashara, akawaambia, Mtu atakaye kuwa wa kwanza, huyu anapaswa kuwa wa mwisho kuliko wote, na mhudumu wa wote.

1Wakor. 6:9 Wasio na haki hawataurithi ufalme wa Mungu.

Waga. 5:21 Husuda, uuaji, ulevi, karamu za fujo, na yanayofanana na haya ... watu wafanyayo mambo kama haya hawataurithi ufalme wa Mungu.

Waefe. 5:5 Maana neno hili mnalijua, kwamba hakuna mwasherati [na wakala wa uasherati], wala mchafu, wala mtu wa tamaa, yaani mwabudu sanamu, aliye na urithi katika ufalme wa Kristo na wa Mungu.

Yak. 2:5 Sikilizeni, ndugu niwapendao, Mungu hakuwachagua maskini wa dunia wawe matajiri wa imani na warithi wa ufalme aliowaahidia wampendao?

Matt. 19:23 Yesu akawaambia wanafunzi wake, Amin, nawaambieni, ya kwamba itakuwa ni vigumu kwa tajiri kuingia katika ufalme wa mbinguni. 19:24 Nawaambieni tena, Ni rahisi ngamia kupenya katika tundu la sindano, kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu.

War. 14:17 Maana ufalme wa Muugu si kula na kunywa, bali haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu.

***Utadumu Milele***

2Sam. 7:12-13 12 Nawe siku zako zitakapotimia, ukalala na baba zako, nitainua mzao wako nyuma yako, atakayetoka viunoni mwako, nami nitaufanya imara ufalme wake.
13 Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa jina langu, nacho kiti cha enzi cha ufalme wake nitakifanya imara milele.
Isa. 9:7 Ongezeko la enzi yake na la amani halitakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele. Ari ya Bwana wa majeshi ndiyo itakaotenda hayo.
Dan. 2:44 Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele.
Luka 1:33 Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele; wala ufalme wake hautakuwa na mwisho.
Waebr. 12:28 Basi, kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutikiswa, tuwe na shukrani, ili kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, katika unyenyekevu na kicho:
Dan. 7:18 Lakini watakatifu wake Aliye juu wataupokea ufalme, na kuumiliki huo ufalme milele, naam hata milele na milele… Ufalme wake utakuwa ni ufalme wa milele, na mamlaka zote zitamtumikia na kumtii.

Hivyo tumeona kwamba Ufalme ulitakiwa kufika katika majira ya *kizazi cha baadhi* ya wafuasi wa Yesu. Ufalme ulifika / ulikuja ukiunganishwa na uharibifu wa Yerusalemu “wakati mambo haya yote yalipotokea” na Yesu akaja kuhukumu kati ya kondoo na mbuzi. Ufalme huu una hulka ya kiroho, nao *utastahamili milele*.

**17 JINSI GANI TUTAFSIRI LUGHA YA UNABII?**
Ikiwa tunajua majira ya kutokea kwa tukio, basi inakuwa rahisi zaidi kumaizi tukio hili ni la aina gani. *Majira* yanapotokea tukio yanasaidia kuelewa *hulka* ya tukio lenyewe. Hili ni jambo la kweli haswa kuhusiana na ujio wa pili na matukio mengine yanayohusika nao. Kama tunajua kwamba ujio huu ulitakuwa kufanyika katika karne ya kwanza kuhusiana na uharibifu wa Yerusalemu katika mwaka 70 B.K., basi tunajua kwamba halikuwa tukio la kuiwasha moto dunia, kuvunjika kwa ulimwengu, kuisha kwa ulimwengu. Badala yake, ulikuwa ni mwisho wa ulimwengu wa Uyahudi ya Agano la Kale.

Kuna wingi wa aina ya lugha ya “mwisho-wa-dunia” inayotumika katika Biblia ambayo kwa mtazamo wa juu juu tu itaonekana kama vile inazungumzia kuisha kwa ulimwengu unaoonekana,

wakati kiuhalisia inazungumzia mabadiliko ya enzi (kutoka enzi moja kwenda nyingine). Kiebrania cha Agano la Kale kilizifasili dunia hizi mbili kama “ulimwengu huu” (*olam ha-zeh*) na “ulimwengu ujao” (*olam ha-bah*). Kiyunani cha Agano Jipya kinaufasili ulimwengu huu kama “enzi hii” (*touto aioni*) na “enzi inayokaribia kuja” (*mellontos aionos*). Tazama Matt. 12:32; Waefe. 1:21; Waebr. 8:5. Kulikuwa ni kubadilika kwa Mfumo wa kale wa Kiagano wa dunia kuingia katika Mfumo mpya wa Kiagano wa dunia, na si mwisho wa ulimwengu.

Zaidi ya hapo, kiasi kikubwa cha lugha inayotumika katika Maandiko kufasili Siku ya Bwana na ujio Wake akiambatana na malaika wake katika mawingu ya utukufu, ni *lugha ya kuonekana kwa Mungu, lugha ya ki-theofania*. Lugha hii inafasili kuonekana kwa Mungu (katika sura fulani) akija na malaika wake ili kuwapatia thawabu watakatifu wake na kuwahukumu adui zake (tazama Isa. 13:6-19; Ezek. 30:1-12; Yoeli 1:15–2:11; Zefa. 1:7- 14). Hii siyo lugha ya kimethali, ya kielelezo tu. Lugha hii inazungumzia mwingiliano halisi, unaoonekana, wenye hisia kati ya ulimwengu unaoonekana na usioonekana. Tunaposikia au kusoma lugha kama “mbingu zikafunguka,” hii anafasili kufunguka kweli kweli kwa himaya isiyoonekana ili watakatifu waweze kuona kitu ambacho kwa kawaida hakionekani,

Hii ni lugha inayohusisha mbingu na nchi. Kosmolojia ya Biblia ni elimu ya uhusiano na mwingiliano kati ya vitu vilivyoko katika ulimwengu unaoonekana na ulimwengu usioonekana. Waandishi wa Biblia wanaitumia sana lugha hii, haswa katika matukio ya *theofania* (kuonekana kwa Mungu) na *angelophanies* (kuonekana kwa malaika). Mahala popote katika maandiko ambapo tunasoma kuhusu kuingiliana kunakoonekana au kwa njia ya hisia kati ya ulimwengu unaoonekana na ule usioonekana, mwiingiliano huo utafasiliwa katika lugha ya kosmolojia. Hii siyo tu lugha ya alama au inayoelezea maafa makubwa.

Mfano mzuri wa theofania ni pale wingu la utukufu la uwepo wa Mungu liliposhuka juu ya mlima wa Sinai - Horebu – katika moto (Kut. 19:16ff). Theofania ile ilionekana na ilisikika. Wana wa Israeli waliliona wingu la utukufu wakati wa mchana na nguzo ya moto wakati wa usiku. Mara tu kabla ya mfalme Solomoni hajaomba katika siku ya kuwekwa wakfu kwa hekalu lake, tunasoma kwamba wingu la utukufu la uwepo wa Mungu lilionekana likijaa ndani ya hekalu na kukaa katika patakatifu pa patakatifu (1Wafa. 8:1-11). Elisha alimwona kwa macho yake Eliyah akichukuliwa katika magari ya moto kuelekea mbinguni (2Wafa. 2:11-12). Elisha na mtumishi wake Gehazi waliyaona kwa macho yao majeshi ya malaika yakiuzunguka mji wa Dotani yakiwalinda wao (2Wafa. 6:17).

Hayo yalikuwa matukio halisi ya theofania na angelo-fania ambayo Mungu aliruhusu watu Wake wayaone kwa macho, wayasikie kwa masikio yao, na pia kuyapitia kwa hisia zao. Ulimwengu haukufikia mwisho wake wakati wa matukio yale. Na hii ni aina ile ile ya lugha ambayo Yesu aliitumia katika kufasili ujio Wake pamoja na malaika katika utukufu wa Baba Yake ili kuwapa thawabu wafuasi Wake na kuwahukumu adui zake. Ilikuwa lugha ya ki-kosmolojia iliyofasili matukio halisi ya mwingiliano unaoonekana na kusikika kati ya ulimwengu unaoonekana na usioonekana. Tazama lugha inayotumika katika aya zifuatazo kufasili kuanguka kwa mataifa maovu (na si mwisho wa ulimwengu): Isa. 13; Isa. 24-34; Isa. 51,52; Jer. 4; Ezek. 32; kitabu chote cha Yoeli; Hag. 2; Zef. 1; Zak. 14. Lugha tunayosoma humo kwa hakika inasikika kama Mwisho wa Ulimwengu kwetu sisi tunaoishi katika ulimwengu wa sasa, lakini muktadha wake unaonyesha tu kuhusu ujio wa Mungu ili kuwapa thawabu watu Wake na kuwahukumu adui zake. Ulikuwa ni “Mwisho wa Dunia” kwa yale mataifa ovu aliyoyahukumu, lakini haukuwa mwisho wa sayari hii wala ulimwengu huu. Na lugha hii hii inatumika katika Agano Jipya kufasili kurejea kwa Kristo ili awaokoe watakatifu Wake kutoka katika Dhiki Kuu na kumwaga ghadhabu Yake dhidi ya watesi wao (Wayahudi).

**18 JE, AGANO LA KALE LILIBASHIRI UJIO WA PILI?**

Wengi kati yetu yamkini watajibu “ndiyo” ya haraka kwa swali hili hapa juu bila kutambua maana na matokeo yake. Kama ulijibu “ndiyo,” uko sahihi! Wakristo wamejaribu siku zote kuwaridhisha Wayahudi kwamba Agano la Kale lilibashiri Ujio wa Pili na matukio mengine ya majira yale ya mwisho. Aya zifuatazo ni mifano mizuri:

Ayubu 19:25 Lakini mimi najua ya kuwa Mtetezi wangu yu hai, Na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi.

Zab. 96:13 Mbele za Bwana, kwa maana anakuja, Kwa maana anakuja aihukumu nchi. Atauhukumu ulimwengu kwa haki, Na mataifa kwa uaminifu wake.

Isa. 40:10 Tazameni, Bwana Mungu atakuja na uweza, Na mkono wake utatatawala kwa ajili Yake; Tazameni, thawabu yake i pamoja naye, Na ijara yake i mbele zake.

Isa. 66:15 Maana Bwana atakuja na moto, na magari yake ya vita kama upepo wa kisulisuli; ili atoe malipo ya ghadhabu yake kwa moto uwakao, na maonyo yake kwa miali ya moto. 16 Kwa maana Bwana atatimiza hukumu yake kwa moto na kwa upanga wake; nao watakaouawa na Bwana watakuwa wengi.

Isa. 38:16-23 nawe utakuja na kusimama dhidi ya watu wangu Israeli, kama wingu linavyoifunika nchi; itakuwa katika siku za mwisho, nitakuleta upigane na nchi yangu, ili mataifa wanijue, kwani kupitia kwako, Ewe Gogu, nitaonyesha utukufu wangu mbele ya macho yao.
17 Bwana MUNGU asema hivi; Je! Wewe ndiwe niliyemnena katika siku za nyuma kwa vinywa vya watumishi wangu, manabii wa Israeli, waliotabiri siku zile kwa miaka mingi, ya kwamba nitakuleta upigane nao?
18 Itakuwa katika siku hiyo, Gogu atakapokuja kupigana na nchi ya Israeli, asema Bwana MUNGU, ghadhabu yangu itapanda.
19 Kwa maana katika wivu wangu, na katika moto wa ghadhabu yangu, nimenena, Hakika katika siku ile kutakuwako tetemeko kubwa katika nchi ya Israeli;
20 hata samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama wa kondeni, na vitu vyote vitambaavyo juu ya nchi, na wanadamu wote walio juu ya uso wa nchi, watatetemeka mbele ya uso wangu; nayo milima itatupwa chini, na magenge yataanguka, na kila ukuta utaanguka chini.
21 Nami nitaita upanga, uje juu yake katika milima yangu yote, asema Bwana MUNGU; nao upanga wa kila mtu utakuwa juu ya ndugu yake.
22 Nami nitamhukumu kwa tauni, na kwa damu; nami nitanyesha mvua ifurikayo, na mvua ya mawe makubwa sana, na moto na kiberiti juu yake, na vikosi vyake, na watu wa kabila nyingi walio pamoja naye.
23 Nami nitajitukuza, na kujitakasa, na kujidhihirisha, mbele ya macho ya mataifa mengi; nao watajua ya kuwa mimi ndimi Bwana.

Dan. 12:1-3 Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati huo; na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile.
2 Tena, wengi wa hao walilala katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele.
3 Na walio na hekima watang'aa kama nuru ya anga; na hao wanaowaongoza wengi katika haki watang'aa kama nyota milele na milele.

Yoeli 3:11-16 Mje, enyi wapagani wote, wa pande zote, jikusanyeni pamoja; na huko wateremshe mashujaa wako wote, Ee Bwana.
12 Mataifa [ya wapagani] na wainuke, wakapande juu katika *bonde la Yehoshafati; maana huko ndiko nitakakoketi niwahukumu mataifa yote yaliyo pande zote.
13 Haya! Ingizeni mundu, maana mavuno yameiva; njoni, kanyageni zabibu; kwa maana mnara umejaa, mapipa [ya mvinyo] nayo yanafurika; kwani uovu wao ni mwingi sana.
14 Makutano makubwa, makutano makubwa, wamo katika *bonde la maamuzi! Kwa maana siku ya Bwana i karibu, katika bonde la **maamuzi. **Hukumu.
15 Jua na mwezi vitatiwa giza, na nyota zitaacha kuangaza.
16 Naye Bwana atanguruma toka Sayuni, atatoa sauti yake toka Yerusalemu; na mbingu na nchi vitatetemeka; lakini Bwana atakuwa tumaini la watu wake, na ngome ya wana wa Israeli.

Zak. 14:2-5 Hapo ndipo atakapotokea Bwana, naye atapigana na mataifa hayo, kama vile alipopigana zamani siku ya vita.
4 Na siku hiyo miguu yake itasimama juu ya mlima wa Mizeituni, unaoelekea Yerusalemu upande wa mashariki, nao mlima wa Mizeituni utapasuka katikati yake, upande wa mashariki na upande wa magharibi; litakuwako huko bonde kubwa sana; na nusu ya mlima ule utaondoka kwenda upande wa kaskazini, na nusu yake itaondoka kwenda upande wa kusini.
5 Nanyi mtakimbia kwa njia ya bonde la milima yangu; kwa maana bonde lile la milima litaenea hata Aseli; naam, mtakimbia, kama vile mlivyokimbia mbele ya tetemeko la nchi, siku za Uzia, mfalme wa Yuda; na Bwana, Mungu wangu, atakuja, na watakatifu wote pamoja naye.

Malaki 4:1-6 Kwa maana, angalieni, siku ile inakuja, inawaka kama tanuru; na watu wote wenye kiburi, nao wote watendao uovu, watakuwa makapi; na siku ile inayokuja itawateketeza, asema Bwana wa majeshi; hata haitawaachia shina wala tawi.
2 Lakini kwenu ninyi mnaoshikwa na hofu mkilisikia Jina langu, jua la haki litawazukia, lenye uponyaji katika mbawa zake; nanyi mtatoka nje, na kucheza-cheza kama ndama wa mazizini.
3 Nanyi mtawakanyaga waovu; maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu; katika siku ile niifanyayo, asema Bwana wa majeshi.
4 Ikumbukeni torati ya Musa, mtumishi wangu, niliyomwamuru huko Horebu kwa ajili ya Israeli wote, naam, amri na hukumu.
5 Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya Bwana, iliyo kuu na ya kuogofya.
6 Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana.

Kama aya hizi zinabashiri jambo ambalo halijatokea bado, basi tuna tatizo kubwa! Katika Luka 21:22, Yesu alisema kwamba unabii wote wa Agano la Kale utatimizwa kabla Yerusalemu haijaangamizwa hapo mwaka 70 B.K. Hii ina maana kwamba matukio yote yaliyobashiriwa katika aya za hapo juu lazima yalitimia! Je, aya hizo [hapo juu] zinazungumzia “ujio katika uweza na utukufu mkuu pamoja na malaika” kama unavyosema ubashiri katika Agano Jipya?” Kwa hakika, ndiyo!

Agano Jipya linathibitisha kwa wazi kabisa kwamba matukio haya ya majira ya mwisho yalibashiriwa katika Agano la Kale. Hapa kuna mifano michache: Matendo. 3:19-24; Matendo. 25:6-8, 22; 1Pet. 1:1-12; and 2Pet. 3. Petro alipokuwa akifundisha katika hekalu kuhusiana na mambo yaliyokuwa yakitokea mbele ya macho yao (“siku hizi” – Matendo. 3:24), anasema kwamba mambo haya yote (pamoja na kurudi kwa Kristo) yalibashiriwa na manabii wa Agano la Kale (Matendo 3:21,24). Paulo alisema kwamba yeye alifundisha tu mambo ambayo “mitume na Musa walisema yatatokea” (Matendo 26:22), nasi tunajua kwamba mara nyingi alizungumzia Ujio wa Pili na matukio mengine ya nyakati za mwisho (1Wakor. 1:7f; 15:23; Wafi. 3:20; Col. 3:4;

1Wathess. 1:10; 2:19; 3:13; 4:13-18; 5:2,23; 2Wathess. 1:7,10; 2:1,8; 1Tim. 6:14; 2Tim. 4:1,8,18; Tit. 2:13; Waebr. 9:28; 10:37). Baada ya kujadili “wokovu ulio tayari kufunuliwa katika majira ya mwisho” (1Pet. 1:5), ambao ungekuja ukihusiana na kurejea kwa Kristo (1Pet. 1:7), Petro anasema kwamba mambo yote haya ya majira ya mwisho yalibashiriwa na manabii wa Agano la Kale (1Pet. 1:1-11)! Petro alitilia mkazo ukweli (2Pet. 3) kwamba yeye alikuwa akiwakumbusha tu juu ya kile Mungu alikwishawaahidi katika Agano la Kale. Anataja “ujio” (aya ya 4), “Siku za Mwisho” aya ya 3, “Siku ya Hukumu” (aya ya 7), “Siku ya Bwana” (aya ya 10) na matukio mengine ya siku za mwisho. Ikiwa tunakubali kuhusu majira ya kutimia kwa mambo haya au la, kitu kimoja ni cha uhakika: Manabii wa Agano la Kale walitabiri matukio haya yote ya majira ya mwisho. Na Petro anasema kwamba “Mwisho” wa mambo haya yote ya mwisho ulikuwa unakaribia haraka (1Pet. 4:4,17). Aliandika mambo haya katika mwaka 63 B.K., kabla tu ya mateso ya Nero dhidi ya Wakristo (64 B.K.) na kuanza kwa vita ya Wayahudi dhidi ya Warumi (66 B.K.). Hivyo, Ujio wa Pili ni lazima ulikwishotokea, kwani hili ni moja kati ya matukio yaliyobashiriwa katika Agano la Kale ambayo yalipaswa kutokea kabla ya kuangamia kwa Yerusalemu katika mwaka 70 B.K!

Agano la Kale lina zaidi ya idadi kadhaa ya unabii ambao umesambazwa hapa na pale katika vitabu vyake kuhusiana na Ujio wa Pili. Kiini chote cha wokovu katika Agano Jipya kimelenga kwa Kristo na kile Atakachofanikisha Msalabani na katika Ujio wa Pili. Na tunahitaji kukumbuka kwamba Parousia (Ujio wa Pili) si tukio la siku moja. Wayunani walilitumia neno “parousia” kumaanisha ziara ya muda mrefu ya mtawala kutoka katika familia ya kifalme. Tukichukua mfano wa Nero, parousia yake ya Uyunani (Greece) ilichukua zaidi ya mwaka. Ukiiweka dhana hii akilini mwako, inakuwa rahisi kuona kwa nini ujio wa Kristo kwa ajili ya kutoa thawabu na hukumu ulichukua takriban miaka minne (kutoka 66 B.K. mpaka 70 B.K.).

## 19 KWA NINI WAYAHUDI WALIANGAMIZWA?

Katika mkusanyiko wa aya tulizonukuu hapa chini, tunaweza kuona kwa nini Mungu alitoa hukumu dhidi ya taifa la Kiyahudi mwaka 70 B.K. Ilibashiriwa katika Agano lote la Kale, na ikatimia katika karne ya kwanza pale Kristo alipokuja kuwaokoa watu Wake na kuwaangamiza adui zake. Sehemu ya kwanza ya aya hizi inatoka katika Agano la Kale, mahususi kutoka katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati, ambapo Musa aliwaonya wana wa Israeli kuhusu kitakachowasibu katika *siku za baadaye* ikiwa watalivunja Agano. Sehemu ya pili ya nukuu hizi inatoka katika Agano Jipya, ikidhihirisha kwamba ubashiri wa Musa ulitimia mpaka nukta ya mwsiho katika ujio wa Kristo na kusimikwa kwa Ufalme wa Milele:

> Na Musa akawakusanya wana wa Israeli na kuwaambia, “Mmeona yote ambayo Bwana ameyafanya mbele za macho yenu katika nchi ya Misri dhidi ya Farao na watumishi wake wote na nchi yake yote … **Kama mioyo yenu itageuka** na [kama] hamtatii … Ninawatamkia siku ya leo kuwa **mtaangamia kwa hakika.** ,,, kwani ninajua ya kwamba baada ya kifo changu **mtafanya mambo maovu** na kugeuka kutoka katika njia niliyowaamuru; na **maafa yatawatokea katika siku za baadaye …** Wametenda maovu dhidi Yake, hawa si watoto Wake, kwa sababu ya dosari yao; lakini ni kizazi potovu na kilichoharibika. Na Bwana akaona hili, na akawatoa mbele za uso Wake kwa sababu ya kukasirishwa na watoto Wake. Halafu akasema, “Nitauficha uso wangu mbele za macho yao, **nitaona nini kitakuwa mwisho wao,** kwani **hiki ni kizazi kilichopotoaka,** wana ambao ndani yao hakuna uaminifu. Wamenifanya Mimi nione wivu juu ya kitu ambacho si Mungu; wamenichokoza na kunikasirisha kwa sababu ya sanamu zao, hivyo **nami nitawafanya waingie wivu juu ya watu ambao si taifa … furahini na watu Wake, Enyi mataifa;** kwani atalipiza kisasi cha damu ya watumishi Wake, na **atalipa kisasi** dhidi ya adui zake, na kulipa makosa dhidi ya nchi Yake na watu Wake. … Hakuna kama Mungu wa

> Jeshuruni, **Ajaye kukusaidia akiwa amepanda juu ya mbingu,** na akipita mawinguni katika utukufu Wake. Mungu wa milele ndiye **makazi yako**, na mikono ya milele I chini yako; Naye **alimfukuza adui kutoka usoni pako,** na akasema, “Angamiza!” (Deut. 29:2; 30:17-18; 31:29; 32:5,19-21,43; 33:26-27).
>
> “… Vivyo hivyo nanyi, **myaonapo haya** yote, basi mjue ya kuwa **yu karibu**, tena milangoni. Amin, nawaambieni, **Kizazi hiki** hakitapita, bila haya yote kutimia.” “Kwa kuwa **ahadi hii ni kwa ajili yenu, na watoto wenu, na watu wote walio mbali,** na wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu.” Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya, akisema, “**Jiokoeni kutoka kizazi hiki chenye ukaidi!**” Dhiki na uchungu juu ya kila moyo wa mwanadamu atendaye uovu, kwanza Myahudi na Myunani pia; Bali utukufu, heshima, na amani kwa kila mtu atendaye mema, Myahudi kwanza na Myunani pia … Atukuzwe Mungu, Baba yake Bwana wetu Yesu Kristo, **aliyetubariki kwa baraka zote za kiroho**, katika milki za mbinguni, ndani ya Kristo; ... Katika yeye tuna ukombozi kwa damu yake, msamaha wa dhambi zetu ...  Baada ya kutujulisha siri ya nia yake, kwa kadiri ya mapenzi yake, aliyoyakusudia ndani yake Mwenyewe, Ya kwamba wakati mkamilifu utakapowadia atajumlisha vitu vyote viwe umoja katika Kristo, vitu vilivyo mbinguni, navyo vilivyo duniani. … Ni nani atakaetutenga na upendo wa Kristo? … Katika mambo haya yote **tunashinda, na zaidi ya kushinda**, kwa yeye aliyetupenda. (Mattt 24:33-34; Matendo 2:39-40; War. 2:9-10; Waefe. 1:3- 10; War. 8:35-37).

Wayahudi wasioamini walikatwa kutoka katika urithi wao na kuangamizwa, wakati waliobaki kati ya Wayahudi waaminifu, pamoja na watu wa Mataifa walioamini, wakarithi baraka za agano (War. 9-11; haswa 11:17-24). Hivyo, kusimikwa kwa Ufalme wa Milele wa Kristo wakati wa kuharibiwa kwa Yerusalemu mwaka 70 B.K. kulikuwa ni kutimizwa kwa mambo yote yaliyoahidiwa kwa wateule wa Mungu, Israeli halisi ya kiroho, ambayo ilijumuisha wote, Wayahudi waaminifu na Watu wa Mataifa walio waaminifu (cf. War. 2:28-29; 9:6-8; 9:22-24; 11:5-7).

**20 VIPI KUHUSU ISRAELI YA LEO?**

Kutajwa tu kwa uharibifu ule wa mwaka 70 B.K., kunasababisha maswali halali kabisa kati ya Wayahudi. Mwandishi wa kijitabu hiki anapenda kuwahakikishia Wayahudi kwamba yeye hawatupii hatia Wayahudi wa leo kwa kile ambacho baadhi ya wahenga wao walifanya katika karne ya kwanza. Mwandishi hana msimamo wala hisia za kuwapinga au kuwachukia Wayahudi (anti-Semitism) kabisa, na badala yake anafurahia kwa upendo mwingi urithi mkubwa waliouacha kwa wanadamu wote (haswa Wakristo), na ufahamu wenye masikitiko na huruma kuhusiana na adha kuu waliyopitia katika historia ya dunia hii. Ulimwengu huu una mambo mengi ya kujifunza kutoka katika historia na dini yao, na mengi ambayo kwayo tunawashukuru. Mtume Paulo anasema kwamba Israeli imekuwa “kipenzi kwa sababu ya [ma]baba” wa imani yetu, na ni “adui” tu kwa sababu waliikataa Injili, waliwatesa watakatifu na kumwua Mwokozi wetu. Wayahudi ndio “… walioaminiwa kwa kukabidhiwa matamko ya Mungu.” Kama Yesu alivyosema, “… kila mwandishi aliyefundishwa elimu ya ufalme wa mbinguni amefanana na mtu mwenye nyumba atoaye katika hazina yake vitu vipya na vya kale” (Matt. 13:52). Na kupitia kwa Wayahudi ndipo watu wa Mataifa wamepokea ukombozi, kwani, “ukombozi unatoka kwa Wayahudi” (Yoh. 4:22). Lakini inapaswa kuelezwa kwa wazi kabisa kwamba Israeli ya kimwili (Israeli ya kimbari, ya kikabila na ya kitaifa) haina nafasi ya upendeleo au dhamana katika ufalme wa kiroho wa Kristo, bila kujali kwamba wao ni uzao wa kimwili wa Abrahamu au wafuasi wa Sheria ya Musa. Hekalu, ukuhani na dhabihu vilikuwa ni vielezo na ishara za uhalisia wa kiroho tulio nao katika Kristo. Mabaki ya waumini katika Masiha Yesu walio waaminifu, wa Kiyahudi, walipandikizwa upya katika Mzeituni wa Mungu, pamoja na waumini wa Mataifa, ili kuujaza Mti mmoja wa Mzeituni wa “Israeli yote”

(War. 11:17-24; Yoh. 10:16). Masihi Yesu amekamilisha mambo yote katika Yeye Mwenyewe pamoja na Israeli halisi ya Kiroho (Kanisa, Ufalme). Nchi ya leo ya Israeli siyo “nchi ya ahadi ya kiroho,” na wazaliwa wa kimwili wa Abrahamu si “Watu Waliochaguliwa.” Ahadi hizo zote zinatimizwa katika Yesu Kristo na ufalme Wake wa kiroho (“mambo bora zaidi ya mbinguni” - Waebr. 9:23; 11:16; 12:22-28) ambayo Wakristo wote wanafaidika nayo kwa sasa. Waumini wa Kristo ni raia wa *nchi iliyo mbinguni*, na wana hekalu, ukuhani na dhabihu bora zaidi (za kiroho). Dhabihu za kimwili, ukuhani na hekalu, vyote viliandikiwa “kupotea” wakati mbadala wake halisi wa kiroho utakapoasisiwa (Waebr. 7:12,18f; 8:13; 9:8-10; 2 Wakor. 3:7,13; Marko. 2:21f; Wakol. 2:8-23). Futurists wengi (haswa wale wanaoitwa *pre-millenial dispensationalists*) wanaamini kwamba Kristo alishindwa katika mpango Wake wa kusimika ufalme wa hapa duniani, na kwamba Atalazimika kuja tena, kujenga upya hekalu, kurejesha mfumo wa makuhani na dhabihu, na kujaribu tena. Unabii [wote] unaohusiana na kusimikwa kwa Ufalme ulipaswa kutimizwa katika wakati ambao hekalu linasimama na dhabihu zinafanyika, na kwa kuwa wanaamini kwamba ufalme haujafika hapa duniani bado, wanafikiri kwamba hekalu linapaswa kujengwa tena na mfumo wa dhabihu kurejeshwa. [Lakini] hii itafanya kazi ya ukuhani na dhabihu ya Kristo msalabani kuwa haina maana wala haina uweza wowote.

## 21 HII INABADILISHA VIPI MTAZAMO WETU WA ULIMWENGU?

Mtazamo wa ki-futurist ulioenezwa sana na Scofield, Walvoord, Lindsey, LaHaye, Tommy Ice, Grant Jeffrey, Van Impe, na wengine umeleta mkanganyiko mkubwa sana. Tabia ya kudumu ya kuweka tarehe za “mwisho wa dunia / kiyama” imewakatisha tamaa watu wengi sana, na imewapa silaha wakosoaji wengi dhidi ya Ukristo, dhidi ya Yesu Kristo na Biblia. Kila kizazi kinafikiria kwamba chenyewe ndicho “kizazi cha mwisho.” Mitazamo inayotofautiana sana ya unabii wa Biblia siyo tu imewachanganya Wakristo, bali imewakatisha tamaa wengi na kusababisha wengine waasi imani yao kabisa, na kusababisha baadhi wachukue hatua ya kujiua. Hapo mwaka 1988 – 1994, baadhi ya wanawake huko Korea, wakifikiri kwamba unyakuo utatokea kabla ya watoto wao kuzaliwa, walitoa mimba zao.

Mtazamo unaotokana na aina hii ya Futurism ni wa kushindwa (na si ushindi), ni wa kuitoroka jamaa yako, ni wa kujitenga na jamii, na wa kukata tamaa. Mtazamo huu unasababisha watu wafikiri kwamba mambo yanakaribia kwisha, kwa hiyo hakuna sababu ya maana ya kuboresha hali ya jamii kwa ajili ya siku zijazo. Mtazamo huu unaona “hakuna haja ya kuosha vyombo ukingali ndani ya meli inayozama,” Mtazamo huu unaona kwamba mambo ya ulimwengu yataharibika na kuzidi kuharibika kabla ya Mwiaho wa Ulimwengu, hivyo hakuna haja ya kujaribu kuuboresha. Mtazamo wa ki-preterist pekee ndio unatupatia njia sahihi ya muda mrefu ya kuwatia nguvu Wakristo ili waendelee kuupanua Ufalme wa Kristo na kuuboresha ulimwengu katika misingi ya Kikristo kwa ajili ya vizazi vyote vya baadaye.

## 22 VIPI KUHUSU SISI WAKATI HUU?

Kutimizwa kwa eskatolojia katika mwaka 70 B.K. kunatupa maswali kadhaa, kwa mfano: “Tunakwenda wapi kutoka hapa, kama unabii wote umetimizwa? Kuna kitu gani kilichobaki kwa ajili yetu siku za leo? Mtazamo wa Ki-preterist unabadilisha vipi namna tunavyotakiwa kuishi hapa duniani?” Matukio ya ufufuo na hukumu yaliyitokea mwaka 70 B.K. yalikuwa ni ya mara-moja tu (na si ya kurudiwa tena) kama ilivyokuwa kwa Msalaba na Ufufuo wa Kristo. Na, kama Msalaba, matukio hayo yana faida na maana-dokezi (implications) kuu kwa ajili ya Wakristo katika milele yote. David Chilton mara nyingi alisisitiza dondoo hii muhimu kwa kunukuu Isaya 9:6-7 katika kila mwisho wa barua-pepe alizotuma:

> 9:6 Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume; Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa Amani.
> 9:7 Ongezeko la enzi yake na la amani halitakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele…

Ni aina gani ya "ufalme," "enzi," na "amani" aliyokuwa akizungumzia Isaya hapa? Je, ni aina hiyo hiyo ya ufalme aliokuwa anamaanisha Bwana Yesu pale aliposema, "Ufalme wangu si wa ulimwengu huu … [wala si] wa hapa" (Yoh. 18:36)?

Maandiko katika Eze. 47 na Ufu. 21 – 22 yanaeleza hulka ya Ufalme huu unaoendelea. Unafanana na mto wenye maji safi unaotoka katika upeo / kilele cha hekalu jipya la kiroho (Kanisa) ambalo Kristo alianza kulijenga katika Siku za Mwisho, ambao unaongezeka katika upana na kina chake kwa jinsi unavyosafiri mbali zaidi kutoka Yerusalemu. Unaendelea kukua na kuongeza athari yake juu ya tamaduni zote za ulimwengu. Kristo alisema kwamba unafanana na chachu, au mbegu ya haradali. Unaanza kidogo sana na unaonekana kwa shida hapo mwanzo, lakini hatimaye hukua na kufikia nguvu iliyo vigumu kupingika, ya kiroho na kitamaduni. Na katika kingo za mto huu wa uhai panamea mimea yenye matunda matamu na harufu ya kupendeza, mimea inayotoa maskani na uponyaji kwa mataifa yote. Mataifa yote yanatembea kwa mwanga wa ufalme huu na wanaleta utukufu wao katika ufalme huu, na wanaponywa na ufalme huu. Hii inaonyesha kwamba ufalme huu utashinda katika uvamizi wake dhidi ya tamaduni na mataifa yote, ukitoa utukufu ***"katika vizazi vyote, [katika] ulimwengu usio na mwisho"** (Waefe. 3:21). Huu ni usitawi unaoendelea wa utawala wetu wa kiroho katika "uumbaji mpya." Baadhi ya mifano ya Bwana Yesu inazungumzia mwanzo mdogo [sana] wa Ufalme, na pia kukua kwake kwa ajabu baada ya hapo. ****Biblia nyingine zina, "katika vizazi vyote, milele na daima.***

Ni muhimu kutambua kwamba historia ya kanisa mara baada ya mwaka 70 B.K. inaonyesha mwanzo ule ule mdogo [sana] wa Ufalme wa Milele unaofasiliwa katika Eze. 47. Wanazuoni wengi wa historia ya kanisa wanazungumzia ukimya, kukosekana kwa shughuli zinazoonekana za Kanisa kwa karibu miongo miwili baada ya kuangamia kwa Yerusalemu. Hii inaonyesha kwamba Ufalme [huu] kwa hakika ulikuwa na mwanzo mdogo sana wa chemchemi ya maji yenye uhai, mwanzoni ukionekana kwa shida sana, lakini ulisitawi na kuwa mto mkuu uliotakasa tamaduni za dunia. Tunapoona maendeleo makubwa ya Ukristo kutoka mwanzo ule mdogo kabisa katika karne ya kwanza, ni nani asiyeweza kushangazwa na kukua kwake! Hakuna utamaduni ulioweza kupinga ushawishi wake baada ya Injili kuingia katika utamaduni huo. Tayari Biblia imekwishatafsiriwa katika lugha zote kuu za dunia, pamoja na lahaja nyingi. Kuna wamisionari wa Kikristo katika kila nchi ya dunia hii. Hatimaye mataifa yote yatabadilishwa kutokana na uweza wake mkubwa wa kubadilisha [watu], katika namna ile ile ambayo ulimwengu wa Nchi za Magharibi ulivyobadilika. Hata hivyo, Ukristo kamwe hautombadilisha kila mtu katika kila utamaduni, kama ambavyo si kila mtu katika nchi ya Marekani alibadilika. Lakini kila utamaduni utaathiriwa na ushawishi wake [angalau] kwa kiasi kikubwa kama ambavyo Marekani iliathiriwa. Na Kristo yuko hapa kwa ajili ya kuishi ndani yetu na katika matendo yetu [mema] milele, akituwezesha kuwa [ma]balozi Wake kwa ajili ya kuwa na ushawishi na utawala wa kiroho kwa ajili ya utukufu Wake.

Misingi yote ya uadilifu, wema, na ya kiroho iliyofunuliwa katika Biblia itaendelea kutumika katika kila kizazi cha historia ya wanadamu. Hulka ya wanadamu haijabadilika na kamwe haitobadilika. Hivyo misingi ya Biblia inayotawala maisha yetu haina sababu ya kubadilika [au kubadilishwa]. Biblia ni kitabu kwa ajili ya historia yote, sasa na katika historia yote inayokuja. Kwa kuwa wanadamu wataendelea kuwako *****"katika vizazi vyote, [katika] ulimwengu usio na mwisho,"

watoto wetu na vizazi vyao vinavyofuata wataendelea kuishi katika ulimwengu huu milele yote. Hii ina maana kwamba inatulazimu kuitunza sayari yetu na kuzitunza rasilimali zilizomo ndani yake, na tuwafundishe watoto wetu kuitawala sayari hii na kuwa watunzaji wake waaminifu.

Kwa kifupi, mtazamo wa ki-preterist ni mtazamo pekee wa kinabii unaotafsiri kwa uaminifu / usahihi maisha YA KALE ya mwanadamu, namna / jinsi ya kuishi kwa haki katika WAKATI ULIOPO, na unawapa VIZAZI VIJAVYO nyenzo sahihi za kuishi maisha yenye faida na yenye kuzaa matunda mema popote watakapoishi katika ulimwengu huu usio na mwisho.

## 23 MAISHA YALIVYO SASA KATIKA UFALME WA MILELE

Kama Kristo alikwisharejea [hapa duniani] na kusimika Ufalme Wake wa Milele, hii ina maana gani kwetu sisi watakatifu tunaoishi leo? Kuna wanaodhani kwamba maisha yetu ya sasa yanapaswa kuwa kama “maisha ya mbinguni.” Lakini huu si wasifu wa maisha katika Ufalme wa Milele ambao Yesu na mitume walitupatia.

Walifundisha mengi kuhusu jinsi maisha yatakavyokuwa pindi Ufalme utakapowadia. Na sasa kwa kuwa Ufalme umewadia, mafundisho yote yanayohusu jinsi ya kuishi ndani ya ufalme yanatuhusu kikamilifu. Umuhimu wake haujapotea kwa sababu ya [matukio ya] mwaka 70 B.K. Badala yake, baada ya mwaka 70 B.K., ufalme ulianza kuwa jambo pekee la muhimu kwetu na linatuhusu katika maisha yetu.

Bwana Yesu alifundisha mifano mingi sana kuhusu jinsi maisha yatakavyokuwa katika ufalme. Baadhi ya mifano hii inahusiana na jinsi maisha yatakavyokuwa mbinguni, wakati baadhi yake inatufundisha jinsi ya kuishi maisha yetu hapa duniani. Ufalme umo katika himaya zote mbili. Hii ndiyo sababu Yesu alitufundisha tusali kwamba ufalme Wake uje kama ambavyo uko tayari huko mbinguni.

Mambo hapa katika maisha [haya] ya kimwili siku zote yamekosa utimilifu na siku zote za usoni yatakosa kuwa timilifu. Utimilifu unapatikana mbinguni pekee. Lakini Ufalme wa Milele ulipowasili hapa duniani mwaka ule wa 70 B.K. ulianzisha mchakato wa kufanya [mambo kuwa] mapya. Na ingawa mambo kamwe hayatakuwa timilifu hapa duniani, habari njema za ufalme zitaendelea kutakasa utamaduni ulioko na kuponya mataifa katika vizazi vyote vijavyo (Ezek 47:8-12; Ufu. 21:24-27; 22:1-2). Hivyo maisha yetu hapa duniani ni maandalizi ya [maisha ya] uzima wa milele huko mbinguni. Hii ndiyo maana tunaamriwa na Maandiko kuutafuta utakatifu hapa duniani, kwani bila ya huo hatuwezi kumwona Mungu (Waebr. 12:14).

## 24 TUMAINI BORA ZAIDI LA UZIMA WA MILELE

Nilipopata habari za mtazamo wa ki-preterist miaka mingi iliyopita, wazo langu la kwanza lilikuwa kwamba hii lazima inatupora ile nafasi yetu ya uzima wa milele mbinguni tukiwa na miili yetu mipya isiyokufa. Lakini nilipoanza kujifunza aya mbali mbali za Biblia zinazofundisha kuhusu ufufuo na mbingu, nikaona haraka sana kwamba hii inatupatia tumaini bora zaidi kuliko [tumaini] nililokuwa nalo kama *futurist*.

Mkristo wa kawaida wa leo anaamini kwamba tunapokufa, miili yetu inaenda kaburini, na nafsi zetu zisizokuwa na miili zinakwenda Hades (kuzimu) ili kungojea ufufuo, ambapo tutarejeshewa miili yetu na tutaishi milele hapa duniani, dunia ambayo *itaumbwa upya*. Lakini dhana hii ya ufufuo na maisha ya baadaye ilikuwa na hali fulani ya kutokuwa na usahihi. Na lilikuwa ni tumaini linalochukua muda mrefu kutimizwa.

Solomoni anatukumbusha kwamba, *"Kinachotarajiwa kikikawia kuja, moyo huugua. Bali haja ya mtu ikipatikana, ni mti wa uzima"* (Mithali 13:12). Kama Msalaba wa Kristo ulitukomboa kutoka Hades (kuzimu), kwa nini watakatifu walazimike kungojea maelfu ya miaka ili wainuliwe tena na kwenda mbinguni?

Kitabu cha Waebrania kinazungumzia "tumaini lililo bora zaidi" (Waebr. 7:19), "ufufuo ulio bora zaidi" (Waebr. 11:35), na "nchi iliyo bora zaidi, nchi iliyo mbinguni" (Waebr. 11:16). Kitu gani kinaweza kuwa bora zaidi ya ufufuo wa miili unaotuwezesha kuishi tena katika dunia hii ya udongo? Mtume Paulo alitujibu swali hili alipofundisha juu ya ufufuo na maisha baada ya ufufuo tutakapokuwa mbinguni.

Kristo alipokuja na malaika zake [ili] kuwaokoa watakatifu wake waliokuwa hai kutoka katika mateso ya Dhiki Kuu, na kumwaga ghadhabu Yake juu ya watesi wao, aliziinua [pia] nafsi zisizokuwa na miili kutoka Hades (kuzimu) na kuwapatia miili yao mipya [isiyoweza kufa tena] iliyokuwa imetunzwa mbinguni kwa ajili yao (1Wakor. 15:37-49; 5Wakor. 5:1). Ufufuo ule wa nafsi kutoka kuzimu ulitokea katika himaya isiyoonekana (Ufu. 20:13-15).

Halafu miili inayokufa ya watakatifu waliokuwa hai *ilibadilishwa* na kuwa miili isiyokufa, kitendo ambacho kiliwaweka katika himaya isiyoonekana pamoja na watakatifu waliofufuliwa (1Wakor. 15:51-52). Halafu makundi yote mawili ya watakatifu (sasa wakiwa kundi moja) wakanyakuliwa na kwenda kukutana na Kristo na kubaki Naye milele katika himaya isiyoonekana ya mbinguni (1Wathess. 4:16-17).

Hii ina maana kwamba *Hades (kuzimu) iliachwa tupu* baada ya ujio wa Kristo. Watakatifu hawaendi hapo tena wanapokufa. Badala yake, tunapokea miili yetu mipya isiyokufa na kupelekwa mbinguni. Kwa kuwa hatupelekwi tena Hades (kuzimu), hatuna haja ya kufufuliwa tena kutoka kuzimu. Hii ina maana ya kwamba ufufuo kutoka kuzimu haufanyiki tena kwa watakatifu. Mara tunapokufa, tunapokea miili yetu mipya na kupelekwa moja kwa moja mbinguni ambako tunaishi milele. Hilo ni "tumaini bora zaidi," na "ufufuo ulio bora zaidi," katika "nchi bora zaidi" ambamo tutaishi milele.

Hili ni tumaini lile lile la kuishi milele ambalo watakatifu wa enzi zote walikuwa nalo. Ni tumaini ambalo watakatifu wale wa karne ya kwanza walikuwa nalo na walilingojea kwa hamu. Na tumaini hilo *lilitimizwa*. Kwa sasa sisi watakatifu hatuna ulazima wa kwenda Hades (kuzimu) kungojea ufufuo kutoka huko. Badala yake, tunapokufa, sisi watakatifu tunapokea miili yetu isiyokufa na kupelekwa mbinguni. Tumaini hilo linapotimizwa, ni tumaini bora zaidi.

## 25 HITIMISHO

Tumeona kwamba mtazamo wa ki-preterist kuhusiana na unabii ndio mtazamo sahihi kama jibu la mashambulizi ya hoja za wa-liberali na watia-shaka dhidi ya Agano Jipya kama ni neno la Mungu [au la]. Kwa hakika, ni ufumbuzi PEKEE na unaoridhisha wa mtanziko huo. Mtazamo huu unatupatia tarehe za uhakika za kumalizwa kwa uandishi wa Agano Jipya, haswa kwa kitabu cha Ufunuo. Hii imetuwezesha kutafsiri kwa urahisi na kwa kujiamini kitabu cha Ufunuo, kwani kufahamu WAKATI wa kutimizwa kwa unabii wake kunatuwezesha kufahamu HULKA ya kutimizwa kwa unabii huu. Tumeonyesha mtanziko (dilemma) mkubwa wa tafsiri unaowakwaza futurists pale wanapojaribu kuigawanya Matthayo 24 katika sehemu mbili za "ujio wa Mwana wa Adamu" unaotenganishwa na maelfu ya miaka. Tumedhihirisha kwamba Kristo alitakiwa kutimiza unabii wote wa Agano la Kale unaomhusu Yeye katika kizazi kile cha karne ya kwanza. Agano la

Kale lilibashiri kurejea Kwake. Kama hiyo haikutokea katika karne ya kwanza, basi Wayahudi wana sababu halali ya kumkana Yesu kama Masihi wao.

Tumetoa ushahidi mwingi wa ki-nyaraka unaoonyesha kutimizwa katika historia kwa unabii ule kutoka Agano la Kale, ulioandikwa na Josephus na waandishi wengine wa historia wa karne ya kwanza. Tumeonyesha mgongano uliomo katika mtazamo wa 'partial preterism', na dhana yenye makosa makubwa zaidi iliyomo katika *creeds* au 'kanuni za imani' [kuhusiana na Ujio wa Pili wa Bwana wetu], na kwamba mtazamo wa ki-preterist ndio pekee una majibu yanayoridhisha na yasiyo na mgongano kuhusiana na maswali magumu [na yasiyoisha] juu ya unabii ambayo yamelisumbua Kanisa kwa karne hizi zote.

Mtazamo huu hauna vipengele dhaifu ndani yake vinavosababisha mgogoro dhidi ya kanuni muhimu na za msingi za Biblia, wala hautusababishii kukosa motisha ya kuishi maisha yetu ya Kikristo kikamilifu. Sote tutapitia mauti (Waebr. 9:27), na hakuna nafasi ya pili [ya kuokolewa] baada ya hapo (Luka 16:26). Ikiwa tunaamini au la, kwamba kuna "kurudi kwa Kristo" katika siku zetu za usoni, bado tunalazimika kuwa tayari kukutana na Kristo uso kwa uso baada ya kifo cha mwili, na kutathminiwa Naye. Hilo linatosha kutupatia motisha ya kutosha kutenda mema ili kuwa "tayari" kwa mkutano huo.

Mtazamo huu wa kutimizwa kwa unabii katika karne ya kwanza unaweza kuwashangaza baadhi ya Wakristo, kwa sababu unamaanisha kwamba Ukristo wa kimapokeo haukuelewa unabii wa siku za mwisho kwa miaka takriban 2000 ya mwanzo wake. Wale wanaofikiri "kanuni za imani" hazina makosa, zimetoka kwa Mungu, na zina mamlaka, wataudhiwa na kauli hii. Lakini mtanziko unabaki. Mwisho wa yote, "tunahitaji kuamua." Je, tutakana ukweli kwamba Yesu na waandishi wa Agano Jipya waliongozwa na Mungu ili tuendelee kusisitiza kwamba wahenga wa Kanisa na kanuni / *creeds* ambazo zimeandikwa na wanadamu ni sahihi, au tutathibitisha usahihi wa Yesu na waandishi wa Agano Jipya na kusahihisha tafsiri zilizokuwa na makosa za Kanisa la historia na mapokeo yetu? Sehemu ya pili ya swali hili ndiyo inatoa uamuzi pekee ulio sahihi.

Hivyo, kinachosemwa na wahenga wa Kanisa na *creeds* / kanuni [walizoziandika] hakina umuhimu wowote ikiwa Agano Jipya lina makosa. Kama ubashiri wa Agano Jipya kuhusu kurejea kwa Bwana Yesu katika kizazi kile ulikuwa si sahihi, basi imani yote ya kihistoria tuliyoipokea kutoka kwa wahenga wa Kanisa haina maana wala thamani katika kiini chake. Lakini ikiwa ubashiri wa Agano Jipya ulikuwa sahihi, basi hii ina maana tu kwamba tafsiri [na uelewa] wa wahenga wa Kanisa (ambao hautufungi) ulikuwa na makosa. Imani yetu haiwezi kutikisika kama wahenga wa Kanisa walikosea katika kutafsiri matukio ya wakati ule pamoja na Maandiko yaliyoelekeza macho yao katika matukio yale. Lakini imani yetu hii inavurugwa kabisa ikiwa Yesu na waandishi wa Agano Jipya walikosea katika ubashiri wao. *Huu ni mtanziko ambao Ukristo unapaswa kukabiliana nao na kuutatua kwa haraka sana.*

Waliberali, Watia-shaka, na wakosoaji wengine wataendelea kumshambulia Yesu katika dondoo hii. Vita ilianza zaidi ya karne mbili zilizopita katika vyuo vya Wakosoaji wa Ulaya. Mtazamo wa ki-preterist uliingia katika utetezi wa imani wakati huo, katika uandishi wa *ki-conservative* wa wanazuoni kama J. S. Russell na wengine. Katika miaka 100 iliyopita [utetezi huu] umeshika kasi kubwa kama *ufumbuzi pekee wa kuaminika* dhidi ya mtanziko unaoletwa na Waliberali, Watia-shaka, na wakosoaji. Ipe imani yako msukumo na nguvu kubwa kwa kujifunza mtazamo wa ki-preterist.

=0=

If you have questions about any of this, feel free to email us here at the International Preterist Association (preterist1@preterist.org). You might also wish to browse our website to see all of the books and media that are available there (www.preterist.org). Let us know how we may be of greater service to you in your studies of God's Word.

Kama una maswali kuhusu jambo lolote lililojadiliwa katika kijitabu hiki, au jambo linalohusiana, tumia anuani za E-mail zifuatazo kuuliza:

preterist1@preterist.org
rk@sayuni.co.tz

Unaweza pia kuendelea kujisomea vitabu, machapisho, na media nyinginge kutoka:

www.preterist.org

=0=

Maoni ya Mtafsiri, Respicius Kilambo:

Kwa mtazamo wangu, Ukristo (Christianity) bado ni dini changa sana. Biblia yetu ina takriban miaka 4,500 tu tangu ianze kuandikwa, na mchakato wa uandishi wake uliisha takriban miaka 2000 iliyopita. Na kabla ya hapo Mungu alikuwa akiwaongoza watu Wake kwa mapokeo ya mdomo na kwa kauli za moja kwa moja (Waga. 3:19; Waebr. 1:1-2). Kuna miongozo mingi iliyomo ndani ya Biblia ambayo bado kabisa hatujaanza hata kuielewa. Na aya za Isaiah 45:17-18 na Waefeso 3:20-21 zinadokeza kwamba ulimwengu hauna mwisho. Hukumu ipo, lakini mwisho, la!

Kwa hakika Sayansi imeanza kuona kwamba ulimwengu huu hauna mwisho, ingawa sisi Wakristo hatuwezi kutegemea kauli za wanadamu kama mwongozo wetu. Tutaongozwa na Biblia pekee, hata katika juhudi zetu za kisayansi. Ukristo ndiyo dini itakayoiongoza dunia hii katika siku za usoni [mfano wa Ufalme katika maendeleo ya kumea na kukua kwa mti wa haradali, na mifano mingine ya Ufalme wa Mbinguni]. *Injili ilitangazwa katika ulimwengu wote wa karne ya kwanza kabla ya 70 B.K*. Lakini baada ya hapo dunia iliingia katika enzi nyingine nyingi, na watu wameongezeka sana. Ukristo ndio uliowezesha usitawi uliofanyika katika bara la Ulaya na Marekani ya Kaskazini katika takriban karne 8 zilizopita. Uhuru unaotokana na matumizi ya Sheria ya Mungu ndio pekee unaowezesha maendeleo ya kweli na endelevu kwa mwanadamu. Mwanadamu anapoacha Sheria ya Mungu matokeo yake huwa mabaya, kama ambavyo hali ya nchi za Ulaya na Marekani inavyodhihirisha leo hii.

Narudia tena; Ukristo bado ni mchanga sana. Tuna safari ndefu ya kwenda usoni kwetu. Ndugu yangu, usichoke kujifunza neno la Mungu! Usichoke kuenenda kwa kuongozwa na neno la Mungu!

https://sayuni.co.tz